MKAKATI WA OXFAM BARANI AFRIKA
2025 - 2030

# AFRIKA YENYE USAWA



Picha ni kwa hisani ya: Eyeris Communications/Oxfam

## MSINGI WA UBUNTU ('NIPO KWA SABABU TUPO')

# YALIYOMO

**Dibaji** .......... 4

**Muhtasari** .......... 5

**1.0 Utangulizi** .......... 6

**2.0 Sisi ni kina nani na tumeitwa kufanya nini** .......... 8

**3.0 Afrika - hali ya bara letu** .......... 10

**3.1 Ukuaji wa uchumi ambao umewaacha watu wake nyuma** .......... 12

**3.2 Utawala Barani Afrika – mienendo inayotia wasiwasi** .......... 14
Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063 - matumaini kwa Afrika
Demokrasia na nafasi za kiraia - vikwazo hatari
Uhamiaji - shinikizo lililochanganywa na fursa
Haki za kidijitali
Huduma za umma kitovu cha ukosefu wa usawa

**3.3 Udhaifu na migogoro inayodhoofisha maendeleo** .......... 17
Migogoro
Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa
Ukosefu wa uwekezaji katika kilimo

**3.4 Ukiukaji wa haki za wanawake na udhalimu wa kijinsia unaendelea kuzuia maendeleo** .......... 19

**4.0 Nguvu za kuleta mabadiliko (uchambuzi wa uongozi)** .......... 20
Washirika wa kimataifa
Uchumi wenye haki
Utawala unaowajibika na jumuishi
Haki za mabadiliko ya hali ya hewa
Haki za kijinsia
Hatua ya usaidizi wa kibinadamu

**5.0 Malengo ya Oxfam Barani Afrika** .......... 25
Maono yetu
Dhamira yetu
Maadili yetu
Kusudi letu
Mbinu zetu

**6.0 Jinsi mabadiliko yatatokea (nadharia yetu ya mabadiliko)** .......... 28

**7.0 Tutafanya nini (nguzo zetu tano)** .......... 30

**7.1 Uchumi wenye Usawa** .......... 32
Maeneo ya kuzingatia
Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

**7.2 Utawala wenye uwajibikaji na jumuishi** ........ **35**
Maeneo ya kuzingatia
Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

**7.3 Haki za Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa** ........ **39**
Maeneo ya kuzingatia
Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

**7.4 Haki za kijinsia** ........ **43**
Maeneo ya kuzingatia
Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

**7.5 Hatua za usaidizi wa kibinadamu** ........ **46**
Maeneo ya kuzingatia
Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

**7.6 Mtazamo wa Masuala Yanayoingiliana** ........ **50**
Kuondoa ukoloni
Mtazamo wa ufeministi
Kuheshimu haki za kidijitali
Umoja wa watu
Kufikiri kieneo na kutenda kimataifa
Mbinu ya kimfumo
Utekelezaji wa mkakati

**8.0 Athari za mkakati huu kwa Oxfam Barani Afrika** ........ **53**
Kurekebisha njia zetu za kufanya kazi
Mifumo na taratibu
Watu wa Oxfam
Kuchangisha fedha za ufadhili
Mkakati wa kampeni

**9.0 Usimamizi wa hatari** ........ **56**

**Hitimisho** ........ **58**

**Vidokezo** ........ **60**

# DIBAJI

Tunawasilisha mkakati wa Oxfam Barani Afrika 2025–2030, 'Afrika Yenye Usawa', unaoambatana na kiwango kikubwa cha uwajibikaji. Mkakati huu, ulioandaliwa kwa pamoja na kwa kupata mizizi yake katika maadili ya *Ubuntu* ('Nipo kwa sababu tupo'), ni dhamira kali ya kukabiliana na sababu za kimsingi za ukosefu wa usawa katika bara la Afrika.

Licha ya bidii na uwezo wa vijana wa bara la Afrika, bara letu linakabiliwa na vikwazo vingi. Hivi ni pamoja na matukio ya hali mbaya ya hewa, kutengwa kwa wanawake na vijana, ukosefu wa usawa na utawala duni - na hali hizi zinazidishwa na urithi wa kihistoria pamoja na mienendo ya kisasa. Ukweli kwamba mabilionea sita matajiri zaidi barani Afrika wana utajiri ambao ni utajiri unaomilikiwa na nusu ya wakazi wa bara zima[1] unaonyesha jinsi dhamira yetu ilivyo na haraka.

Wakati mkakati huu unachapishwa, ulimwengu na bara zima ziko katika njia panda, zikiwa na fursa na changamoto nyingi. Oxfam Barani Afrika imejitolea kutekeleza jukumu lake halali katika kuleta mabadiliko yenye manufaa katika miaka hii muhimu. Tunaendelea kutoa changamoto kwa mienendo ya mamlaka na uongozi, kukuza uchumi wenye haki, kutoa wito wa utawala wenye uwajibikaji na jumuishi, kutetea haki za kijinsia na haki za hali ya hewa, na kufanya kazi na washirika ili kutoa hatua za kibinadamu zenye ufanisi na zinazofaa maeneo mahususi. Mtazamo wetu unaambatana na Mkakati wa Kimataifa wa Oxfam 2020–2030 na Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063, ambazo zote zinakuza maendeleo ya kijamii, ushirikishaji na ujumuishaji na uendelevu katika mwelekeo wa maendeleo ya bara la Afrika.

Mwanafalsafa wa kisiasa wa Afro-Karibia Franz Fanon aliandika, 'Kila kizazi, lazima, kitoke katika hali ya kutofahamu, kigundue dhamira yake, kiitimize, au kiisaliti.'[2] Mkakati wetu ni jaribio la kutambua na kushughulikia changamoto zinazotukabili, na kufanya hivi kama kikundi, huku tukihakikisha kwamba wafanyakazi katika shirika la Oxfam Barani Afrika, washirika wetu, washirika na Shirika la Oxfam wanatumia uwezo wao kuwezesha suluhisho zenye kuleta mabadiliko.

Mbinu yetu ya kina inalenga mabadiliko ya kimfumo, na kwa hivyo, itatuelekeza katika kutetea mifumo ya haki za fedha, kutetea haki za maliasili, kutetea nafasi za raia, kukuza usawa wa kijinsia na kupunguza mapengo ya maarifa kuhusu mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa. Hivi ndivyo tutakavyoishi na kufanya kazi kwa kuzingatia kanuni ya *Ubuntu*, mbinu ya juhudi za pamoja.

Tunasisitiza umuhimu wa mkakati wetu kuwa wenye kuleta mabadiliko - neno linalotoka kwa Kilatini 'radix', au 'mzizi'. Kuwa mwenye kuleta mabadiliko ni kwenda zaidi ya kutibu dalili; ni kukabiliana na moyo, au mzizi halisi, wa tatizo badala ya dalili zake tu. Suluhisho za kiwango cha juu juu hazitashughulikia changamoto zinazowakabili raia wa bara la Afrika. Kwa bara linalokabiliana na urithi na unyonyaji na unyanyasaji wa kihistoria na mienendo ya sasa inayozalisha ukosefu wa usawa, tunahitaji kutafuta suluhisho ambazo zitaondoa vizuizi vilivyowekwa vya maendeleo. Mbinu hii ya mabadiliko ni muhimu ili kuleta mabadiliko ya haki na ya kudumu; pia ni muhimu kwa kuunda upya mifumo ya kijamii na kiuchumi ambayo itazuia dhuluma za aina hii katika siku zijazo. Hii, kwa maoni yangu, ndiyo njia pekee ya kuhakikisha ustawi wa pamoja na maendeleo yenye usawa katika Afrika.

Tunapoanza safari hii, tunajitolea kuweka juhudi zetu katika kuifanya Afrika kuwa bara la haki na usawa. Mkakati huu ni ushuhuda wa kujitolea kwetu - ni makubaliano ya pamoja yanayoongoza safari yetu ya pamoja ya kuelekea kwenye bara ambalo ukosefu wa usawa ni historia. Hebu tuungane ili kuchukua sehemu yetu ya kazi hii kuu, kwani hatua zetu za pamoja zina uwezo wa kuchangia mustakabali wa usawa kwa wote. Naomba tukabiliane na changamoto zinazotukabili na kuzishinda.

Fati N'Zi-Hassane

Mkurugenzi wa Oxfam Barani Afrika

# MUHTASARI

Mkakati wa Oxfam Barani Afrika (OiA) unatokana na ushirikiano kati ya wadau wote barani, uliowezeshwa na Jukwaa la Afrika (African Platform). Afrika, iliyojaliwa uwezo mkubwa na idadi kubwa ya vijana, inakabiliwa na changamoto zinazoendelea kukua; zikiwa ni pamoja na ukosefu wa usawa, ubaguzi wa kijinsia na wa vijana, mabadiliko ya hali ya hewa na utawala dhaifu. Haya yamezidishwa na urithi wa kihistoria na athari za nje.

Ukuaji wa uchumi barani Afrika hauna usawa, huku kilimo kikichukua jukumu muhimu licha ya hatari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na hali ya kukifanya kilimo kama biashara. Kuongezeka kwa mzigo wa madeni kumezidisha changamoto za kiuchumi, hali inayohitaji suluhisho endelevu. Ukosefu wa haki za kijinsia bado umeenea, ukijikita katika miundo ya mfumo wa ubabedume na mifano ya uchumi mamboleo. Licha ya mifumo ya kisheria, unyanyasaji wa kijinsia unaendelea, hali inayozuia haki sawa za wanawake na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Na licha ya ukuaji wa uchumi, Afŕika inasalia kuwa eneo la pili lenye ukosefu wa usawa mkubwa zaidi duniani, pamoja na kuwa eneo lenye umaskini mkubwa na mazingira magumu. Kushughulikia changamoto hizi kunahitaji mabadiliko katika mienendo utawala na uongozi. OiA inaahidi kuongoza juhudi katika kukabiliana na changamoto za ukosefu wa usawa, kukuza ukuaji jumuishi na kuwezesha jamii za Afrika kuwa na mustakabali mzuri na wenye usawa. Ajenda ya 2063 ya Umoja wa Afrika inatumika kama ramani ya bara la Afrika ya kuleta mabadiliko, ikilenga maendeleo jumuishi na endelevu. OiA itashirikiana na washirika kukuza ushirikiano wa pande nyingi, kufikia na kuimarisha demokrasia ya kikatiba, ulinzi wa haki za kiuchumi, utu kwa wanawake na wasichana, kustahimili hali zinazotokana na mabadiliko ya hewa na utatuzi wa migogoro ifikapo 2030.

OiA inakumbatia kanuni ya *Ubuntu* ('Nipo kwa sababu tupo') na inakuza ushirikiano kati ya washikadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Ofisi za Nchi, Vitengo vya Kikanda na Washirika wa Afrika. Janga la COVID-19 na mabadiliko ya kidijitali yamesababisha OiA kufikiria upya mipaka ya kitamaduni na kubuni mbinu mpya. Mpango wa mkakati wa OiA unaonyesha maono thabiti ya kupambana na ukosefu wa usawa na kukuza haki katika bara zima la Afrika katika kipindi cha miaka sita ijayo. Kwa kuzingatia ushirikiano shirikishi na washirika na mabadiliko ya kimfumo, tunalenga kushughulikia nguzo muhimu za uchumi wenye haki, utawala wenye uwajibikaji na jumuishi, haki za mabadiliko ya hali ya hewa, haki za kijinsia na hatua za usaidizi wa kibinadamu, kwa kutumia lenzi za kuondoa ukoloni, ufeministi, haki za kidijitali na mienendo ya utawala na uongozi, huku tukihakikisha ushirikiano sawa, tukikabiliana na changamoto zinazotokana na mfumo wa ubabedume, tukitetea ufikiaji kwa mifumo ya kidijitali na kuwezesha jamii zilizotengwa. Chini ya nguzo ya uchumi wenye haki, tutatetea mifumo ya haki za fedha, uhuru wa chakula na haki za maliasili, huku tukilenga kupunguza mzigo wa madeni, thamani kwenye mifumo ya kilimo na ugawaji wa mapato wenye usawa. Juhudi za utawala zenye uwajibikaji na jumuishi zitalenga kutetea nafasi za utetezi wa kiraia, kukuza huduma za umma, na kuwezesha harakati za vijana na kijamii kwa ajili ya kuwepo na uwazi zaidi na ushiriki wa raia. Chini ya nguzo ya haki za mabadiliko ya hali ya hewa, OiA inalenga kuziba mapengo ya maarifa, kuathiri mabadiliko ya sera, kukuza ustahimilivu wa jamii za maeneo husika na kutetea ufadhili wa hali ya hewa na uwepo wa usawa. Juhudi chini ya nguzo ya haki za kijinsia zinaweka kipaumbele katika kupambana na unyanyasaji wa kijinsia na kukuza uongozi wa wanawake, haki za kiuchumi, afya na haki za ngono na uzazi. Hatua za usaidizi wa kibinadamu huchukua mkabala wa 'uhusiano wa mara tatu' unaojumuisha juhudi za kibinadamu, maendeleo na ujenzi wa amani huku zikisisitiza mwitikio mwafaka wenye utayari, na kuunganisha mikakati ya uingiliaji kati ya muda mfupi na athari za muda mrefu.

Mafanikio ifikapo 2030 yanatazamwa kwa kuzingatia viashiria madhubuti kama vile mageuzi ya kodi ya kimataifa, mzigo wa madeni uliopunguka, ongezeko la uwekezaji katika huduma za umma, mabadiliko ya sera kuhusu haki za mabadiliko ya hali ya hewa, maendeleo katika usawa wa kijinsia na hatua za mabadiliko katika masuala ya usaidizi wa kibinadamu. Malengo haya yanahitaji mabadiliko ya kimfumo, ushirikiano jumuishi na kujitolea kukabiliana na mifumo ya utawala na uongozi iliyoimarishwa. Utekelezaji wa mkakati huu na kutimiza malengo yake madhubuti utahitaji marekebisho na mabadiliko ya shirika, kwa kuzingatia kazi iliyopo huku tukikuza, kulainisha na kuimarisha juhudi katika maeneo yote ya uendeshaji shughuli. OiA iko tayari kuwa nguvu inayoongoza kwa haki na usawa, ikiendeleza mabadiliko endelevu na uwezeshaji katika bara zima.

# 1.0

# UTANGULIZI

Mkakati wa Oxfam Barani Afrika (OiA) unahusisha ushirikiano kati ya wadau wote wa Oxfam Barani Afrika, unaowezeshwa na Jukwaa la Afrika (Africa Platform). Ufanisi wa OiA katika kutekeleza mkakati huu unategemea mtazamo wetu tofaut; kutumia uwezo na manufaa ya vyombo mbalimbali barani Afrika ili kupata matokeo ya juu zaidi. Licha ya kuwa bara la pili kwa ukubwa duniani kwa kuzingatia ukubwa na idadi ya watu, uwezo wa Afrika bado haujatumiwa. Afrika ikiwa na 40% ya watu wake walio na umri wa chini ya miaka 15,[3] pia ni mwenyeji wa idadi kubwa duniani ya watu wenye umri mchanga zaidi duniani. Hata hivyo, licha ya uwezo huu mkubwa, Afrika bado ina sehemu kubwa ya watu maskini zaidi duniani.

Licha ya miongo miwili ya ukuaji wa uchumi, suala la ukosefu wa usawa bado halijatatuliwa, kama inavyosisitizwa na maelezo kwamba 'Mabilionea sita matajiri zaidi barani Afrika sasa ni matajiri zaidi kuliko asilimia 50 ya Waafrika maskini zaidi wakiwekwa kwa pamoja.'[4] Maendeleo ya Afrika yanategemea uwezo wake wa kushughulikia mielekeo mbalimbali mibaya inayozuia maendeleo yake, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa utulivu wa kisiasa, kuongezeka kwa madeni, ubaguzi wa kijinsia na wa vijana, mabadiliko ya hali ya hewa, changamoto na gharama zinazohusiana na mabadiliko ya nishati, kuongezeka kwa ukosefu wa usawa na utawala dhaifu.

Hata hivyo, Afrika yenye usawa inaweza kupatikana; pia inawakilisha uchaguzi wa kimakusudi. Shirika la Umoja wa Afrika (AU) limeweka Ajenda yake ya 2063 kama ramani ya kubadilisha Afrika kuwa bara lenye nguvu duniani. Ajenda 2063 ni mfumo wa kimkakati wa bara la Afrika, unaolenga kufikia maendeleo jumuishi na endelevu, pamoja na umoja na ustawi. Mkakati huu unajumuisha maono ya Pan-Afrika ya 'bara la raia huru na upeo uliopanuliwa, ambapo uwezo kamili wa wanawake na vijana unafikiwa, huku kukiwa na uhuru kutoka kwa hofu, magonjwa na uhitaji'.[5] Utambuzi wa mabadiliko katika Afrika unategemea kufikia utawala wenye uwajibikaji na jumuishi, ukuaji unaozingatia kuboresha mabadiliko ya hali ya hewa, utulivu wa kisiasa na kijamii, na kuhakikisha uhuru na utu kwa wanawake na wasichana. OiA inaamini kwamba watu wa Afrika ni wajenzi wakuu wa kuleta mabadiliko, na imejitolea kuunga mkono juhudi zao na kutoa majukwaa ya sauti zao kusikika kimataifa.

Kupitia mkakati huu, OiA inaahidi kushirikiana na washirika na kushikilia ahadi zetu za kutoa wito wa utawala wenye uwajibikaji, haki za kiuchumi, haki za rangi, haki za kijinsia, haki za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa na kuondoa ukoloni, hivyo basi kuongoza Afrika. Kufikia 2030, OiA, kwa ushirikiano na washirika wetu na watu wa Afrika, tumejitolea:

- Kukuza na kuunga mkono ushirikiano wa washirika wengi na kukuza demokrasia ya kikatiba kote barani Afrika.
- Kulinda haki za raia, ikiwa ni pamoja na haki za kiuchumi na haki za uwajibikaji kutoka kwa taasisi zao na viongozi wa umma.
- Kuhakikisha utu kwa wanawake na wasichana.
- Kushughulikia na kupunguza hatari za mabadiliko ya hali ya hewa zinazokabili Afrika.
- Kupitisha mtazamo wa kukabiliana na migogoro, unyeti wa migogoro na utatuzi wa migogoro ambao unashughulikia visababishi na mizizi msingi ya migogoro na kwawezesha watu walioathiriwa na migogoro na jamii kuchukua uongozi wa masuala ya migogoro.

# 2.0

# SISI NI KINA NANI NA TUMEITWA KUFANYA NINI

Oxfam Barani Afrika inazingatia kanuni ya Kiafrika ya *Ubuntu* ('Nipo kwa sababu tupo') kwa mshawasha na madhumuni. Kanuni hii inasisitiza mitazamo ya jamii bali sio ya mtu binafsi na kutoa kipaumbele kwa ustawi wa vizazi vijavyo pamoja na ule wa raia waliopo sasa.

Kwa kutambua kwamba hatua za pamoja hutoa athari kubwa na muhimu zaidi, tumejitolea kikamilifu kwa wazo la OiA. Washikadau wote wa Oxfam katika bara hili watatumia mkakati wetu, ikijumuisha Ofisi za Nchi mbalimbali, Vikundi vya Kikanda kama vile Kusini mwa Afrika na Afrika Kaskazini,[6] Ofisi ya Uhusiano ya Umoja wa Mataifa mjini Addis, na Washirika kama vile Oxfam Afrika Kusini na Washirika wa siku zijazo wa Afrika .[7] Jukwaa la Afrika (Africa Platform) linatumika kama ofisi ya usimamizi na uratibu wa kikanda, inayounga mkono ushirikiano kati ya vyombo hivi na uwiano wa shughuli za Oxfam Barani Afrika.

Kwa kushirikiana kimakusudi na kwa ukaribu zaidi na wadau na washirika mbalimbali, OiA inalenga kuimarisha uhalali wetu, ustahiki na uaminifu wetu kama mdau na mshirika. Tumejitolea kutumia kanuni za ufeministi katika mtazamo wetu na kuondoa ukoloni katika desturi na njia zetu za kufanya kazi.

Changamoto zilizoletwa na janga la COVID-19 zimetusukuma kufikiria upya na kuunda upya na kwa pamoja mipaka ya jadi ya kijiografia na lugha. Mabadiliko ya kidijitali pia yanatoa fursa za uvumbuzi. Kwa kuzingatia Mkakati wa Kimataifa na maamuzi ya kimuundo ya Oxfam ya 2030, OiA imewezeshwa kutoa mapendekezo ya ujasiri kuhusu jinsi tunavyofanya kazi katika ngazi ya nchi. Tunaamini kwamba wakati umefika kwa Oxfam kuheshimu ahadi zake kwa wito wa kupigania haki za rangi, haki za kijinsia, haki za kiuchumi, utawala wenye uwajibikaji na jumuishi, haki za mabadiliko ya hali ya hewa na kuondoa ukoloni, kwa kuongoza njia barani Afrika. Tunajua na tutaendelea kufahamu sana haja ya kubomoa na kuvuruga mitazamo na desturi za kikoloni na mfumo wa ubabedume, kiasi cha jinsi tunavyojipanga na jinsi tunavyofanya kazi na wengine katika yale tunayofanya.

Kupanga kazi ya Oxfam chini ya sauti moja barani Afrika, ingawa tutatumia mfumo ufaao wa ushirikiano ili kuunga mkono kazi yetu na serikali za Afrika, Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs) na AU, kufuata kanuni ya ufadhili,[8] ni sharti. Pia ni ombi kutoka kwa jumuiya za kiraia za Afrika, na inalingana na jinsi Afrika inavyohitaji mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali (INGOs) kama vile Oxfam kusalia yakiwa na umuhimu.



Ibado akiwa katika shughuli zake za kila siku akiwatembelea Wakimbizi wa Ndani (IDP's) katika kambi karibu na Oog. Ibado (nguo ya zambarau, miwani) anaishi katika kijiji cha Oog, karibu na Burao huko Somaliland. Anasaidia IDP's ambao ni waathiriwa wa ukame unaoendelea katika Pembe ya Afrika. *Picha ni kwa hisani ya:Petterik Wiggers/Oxfam*

# 3.0

## AFRIKA – HALI YA BARA LETU

Afrika ikawa na idadi kubwa zaidi ya watu wachanga zaidi duniani inayopanuka kwa kasi zaidi, idadi inayokadiriwa kufikia watu bilioni 2.5 ifikapo mwaka wa 2050,[9] Afrika inashikilia fursa nyingi za ukuaji thabiti na jumuishi. Hata hivyo, licha ya uwezo huu mkubwa, sehemu kubwa ya watu wanaoishi katika umaskini mkubwa zaidi duniani wanaishi barani Afrika; hii inaambatana na ongezeko la ukosefu wa usawa na kutengwa.

Kufikia 2020, Waafrika milioni 571 waliishi katika umaskini mkubwa,[10] huku makadirio yakionyesha kuwa ifikapo mwaka wa 2030, Afrika itakuwa na asilimia 88 ya watu maskini duniani[11] na 19.8% ya idadi ya vijana duniani.[12] Takwimu kutoka Tume ya Umoja wa Mataifa ya Kiuchumi ya Afrika (UNECA) zinaonyesha kwamba janga la COVID-19 lilizidisha changamoto hizi, na kuwasukuma karibu Waafrika milioni 55 katika umaskini uliokithiri katika mwaka wa 2020.[13] Hali hii  ilirudisha nyuma zaidi ya miaka 20 ya maendeleo yaliyopatikana katika kupunguza umaskini katika bara zima. Ni muhimu kutambua umaskini kama suala tata linaloathiriwa na masuala mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kihistoria. Mbinu za kukabiliana na umaskini katika bara hili zinapaswa kujumuisha Mataifa ya Afrika pamoja na mashirika ya mashinani na washirika wa kimataifa.




Wachezaji wa kuteleza kwenye barafu wakicheza kwenye msafara wa matembezi ya mabadiliko ya hali ya hewa mnamo Oktoba 13, 2022 huko Maryland, Jimbo la Lagos, Nigeria. *Picha ni kwa hisani ya: Taiwo Aina/ Oxfam*

# 3.1 UKUAJI WA UCHUMI AMBAO UMEWAACHA WATU WAKE NYUMA

Ukosefu wa usawa wa mapato na mienendo ya umaskini barani Afrika inachangiwa kwa kiasi kikubwa na asili ya ukuaji wa uchumi. Ingawa ukuaji wa uchumi una uwezo wa kupunguza umaskini, athari zake katika mgao wa mapato hutofautiana. Ukuaji wa haraka wa miji ni mwelekeo unaojulikana na kuonekana, huku idadi ya watu mijini ikiongezeka kwa kasi zaidi kuliko idadi ya watu wote; hili linahitaji uchambuzi wa kina wa umaskini na mazingira magumu ya kuathirika kwa urahisi. Licha ya mwelekeo huu wa ukuaji wa miji, nusu ya watu wa Afrika, na hasa wale wanaoishi katika umaskini, bado wanajishughulisha na sekta ya kilimo. Kwa hiyo, kuimarisha sekta ya kilimo bado ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Zaidi ya hayo, sekta kubwa isiyo rasmi ya Afrika, ambayo kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani inawakilisha asilimia 85.8 ya ajira,[14] inatoa fursa za maendeleo ya kiuchumi na ajira, hasa kwa makundi yaliyotengwa kama vile Jamii Wenyeji, wanawake na vijana.

Kati ya nchi 54 barani Afrika, 28 zinategemea viwanda vya uchimbaji madini, huku mafuta, gesi, makaa ya mawe na bidhaa za madini zikichangia kati ya 60% na 99.9% ya jumla ya bidhaa zao zinazouzwa nje.[15] Kwa hivyo, sekta ya uchimbaji ina jukumu kuu katika haki za kiuchumi barani Afrika, kwani ina uwezo wa kupata mapato na kupunguza ukosefu wa usawa, kufadhili huduma za kijamii, kuunda ajira na kukidhi mahitaji ya jamii. Hata hivyo, wingi wa maliasili barani Afrika pia umesababisha wasiwasi kuhusu utawala dhaifu na mbaya, mtiririko wa fedha haramu na migogoro kuhusu ugawaji wa rasilimali. Kwa bahati mbaya, changamoto hizi zimechangia kuvunjika kwa taratibu na miundo ya kidemokrasia, hali ambayo imesababisha migogoro katika bara zima. Katika kushughulikia ukosefu wa usawa wa kiuchumi, OiA inatambua umuhimu wa kuunganisha hali tata ya migogoro katika mkakati wake. Mitazamo inayozingatia hali tata za migogoro inahakikisha kwamba mikakati ya uingiliaji kati wa kibinadamu na kimaendeleo inapunguza madhara, inachangia katika kushughulikia sababu kuu za ukosefu wa utulivu, na kusaidia kukuza amani.

Zaidi ya hayo, uchumi wa nchi za Kiafrika umeathiriwa na urithi wa utawala wa kikoloni na mfumo wa kifedha wa kimataifa unaoathiriwa na mawazo ya uliberali mamboleo. Hii imesababisha kupunguzwa kwa udhibiti wa uchumi wa Afrika, hali inayoyaweka masoko ya Afrika katika kwa ushindani usio sawa, na kupunguzwa kwa miundombinu ya kijamii ya mataifa ya Afrika kupitia hatua za kupunguza matumizi ya sekta ya kibinafsi. Kushughulikia masuala haya ya kimfumo ni muhimu kwa ajili ya kukuza haki za kiuchumi na ukuaji jumuishi barani Afrika.

Uchumi na jamii za Kiafrika zinaendelea kutegemea zaidi kilimo; inakadiriwa kwamba bara la Afrika lina mashamba milioni 33 ya wakulima wadogo ambayo sio tu ya uzalishaji wa chakula lakini pia kwa ajili ya kukimu maisha ya Waafrika wengi ambao kazi yao inahusishwa na kilimo.[16] Sekta hii imeonyesha dalili za mafanikio katika miaka ya hivi karibuni, na uzalishaji wa kilimo ukiongezeka kwa wastani wa 13% kila mwaka kati ya 2015 na 2020.[17] Kilimo katika mataifa mengi ya Afrika kinakabiliwa na matatizo mengi, kama vile mbinu za kiteknolojia zilizopitwa na wakati na kilimo cha kutegemea mvua, hali inayokifanya kilimo kuathiriwa sana na atahri za mabadiliko ya hali ya hewa. Zaidi ya hayo, ugeuzaji mwingi wa mifumo ya chakula kwa manufaa ya kibiashara na kupata faida hudhoofisha usalama na uhuru wa chakula wa nchi nyingi. Hali hii inawafanya wakulima wadogo na mifumo ya uzalishaji wa chakula kuwa katika hatari ya kipekee. Matarajio ya Afrika ya kuwa bara jumuishi, lenye ustawi na amani hayawezi kufikiwa ikiwa wakulima wadogo watapuuzwa na mifumo ya chakula kugeuzwa kupita kiasi kwa manufaa ya kibiashara

Afrika inakabiliwa na changamoto kubwa kutokana na viwango vyake vya chini vya ukuaji wa viwanda na uundaji na uongezaji thamani kwenye bidhaa. Bara la Afrika linakabiliwa na viwango vidogo vya watu wenye uwezo kujua kusoma na kuandika, miundombinu duni na upatikanaji mdogo wa nishati, hali inayozuia

ushiriki wake katika uchumi wa dunia na uwezo wake wa kufadhili maendeleo ya 'Mapinduzi ya Nne ya Viwanda'. Huku maeneo mengine yakinufaika na ongezeko la mifumo ya akili bandia na teknolojia ya kidijitali, Afrika imo katika hatari ya kuachwa nyuma zaidi. Pengo la kupitishwa na kutumia kwa teknolojia na uvumbuzi linazidisha tofauti za kiuchumi kati ya bara na kanda zingine, huku bara hili likijitahidi kujumuika katika uchumi wa ulimwengu unaoendeshwa na maarifa. Bila uwekezaji mkubwa katika elimu, miundombinu na teknolojia, Afrika itaendelea kukabiliwa na matatizo katika kufikia ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu.

Kulingana na Shirika la Fedha Duniani (IMF), 'wastani wa uwiano wa madeni katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara imeongezeka karibu maradufu katika mwongo mmoja tu—kutoka 30% ya Pato la Taifa mwishoni mwa 2013 hadi karibu 60% ya Pato la Taifa ifikapo mwishoni mwa 2022', na 'uwiano wa malipo ya riba kwa mapato umeongezeka zaidi kwa mara mbili tangu mwanzoni mwa miaka ya 2010 na sasa ni karibu mara nne ya uwiano katika nchi zenye uchumi wa juu'.[18] Kupanda kwa viwango vya riba kunaongeza gharama, hii inatumia sehemu kubwa zaidi za bajeti za serikali ambazo zingeweza kutengewa huduma muhimu za kijamii kama vile afya, elimu, ulinzi wa jamii, maji na miundombinu. Matumizi haya hayawezi kuendelea kutumika kwa muda mrefu, na hivyo kuzua wasiwasi kuhusu mgogoro wa madeni unaokuja katika nchi nyingi barani.



Amadou Maina, mwenye umri wa miaka 50, anatoka Mkoa wa Ziwa nchini Chad. Mkulima huyu wa natron amekuwa akitazama bila matumaini jinsi ambavyo eneo lake la uchimbaji natron limekuwa likibadilika kuwa janga katika miaka michachae iliyopita. *Picha ni kwa hisani ya: Liga Nassandou/ Oxfam*

# 3.2 UTAWALA BARANI AFRIKA – MIENENDO INAYOTIA WASIWASI

Utawala wenye uwajibikaji na jumuishi ni jambo la msingi katika kushughulikia changamoto nyingi za kijamii, kisiasa na kiuchumi zinazokabili bara la Afrika. Hizi ni pamoja na majaribio ya mapinduzi ya serikali, vikwazo vya nafasi za raia kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari, ukiukaji wa haki za binadamu, kupuuzwa kwa huduma za kijamii za umma, kukandamiza maandamano ya umma, upinzani rasmi kwa vyama vya wafanyakazi na mashirika ya kibinadamu, na ufisadi unaoendelea na uliokithiri. Uhusiano wa kihistoria kati ya serikali na jamii katika nchi nyingi za Kiafrika umekuwa na udhaifu unaotokana na urithi uliopitishwa kutoka kwa ukoloni. Wakati wa enzi ya ukoloni na kipindi kilichofuata cha Vita Baridi, mataifa ya Afrika yalifafanuliwa kwa kiasi kikubwa na mataifa kutoka Upande wa Kaskizini mwa Ulimwengu (Global North), mataifa haya yalitilia mkazo uhusiano wa kidiplomasia badala ya ushirikishaji raia wenye maana.

Kuvunjwa kwa Umoja wa Kisovieti mwaka wa 1991 kuliunda fursa mpya kwa raia wa Afrika na jamii za kiraia kuingiliana na serikali zao. Katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita, kumekuwa na ongezeko la mashirika ya kiraia, huku vuguvugu la wanawake likiibuka kuwa na ushawishi mkubwa. Licha ya maendeleo haya, changamoto nyingi zinaendelea kukua na matukio ya kurudi nyuma yanaonekana. Changamoto hizi ni pamoja na kuongezeka kwa idadi ya vijana ambao wanakabiliwa na kutengwa na ukosefu wa usawa unaoendelea, mambo haya yote yanazuia juhudi za kuimarisha utawala.

## Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063 - matumaini kwa Afrika

Katika miaka michache iliyopita, nchi za Kiafrika zimejaribu kuimarisha umoja kama Umoja wa Afrika (AU), zikiwa na matarajio yao ambayo yameainishwa hivi sasa katika Ajenda ya AU ya 2063. Huu ni mwongozo wa kimkakati wa bara hili, unaolenga ukuaji jumuishi na endelevu unaoandamana na umoja na ustawi. Ajenda hii inawakilisha ndoto ya Pan-Afrika ya bara ambalo raia wanaishi kwa uhuru, fursa zinapanuliwa na bara ambalo uwezo wa wanawake na vijana unatumiwa kikamilifu, katika jamii isiyo na hofu, magonjwa na umaskini. Ajenda ya 2063 inawakilisha mabadiliko makubwa katika mwelekeo wa bara na msingi thabiti wa kuingiliana na wadau wa Kiafrika ndani na nje ya Afrika. Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs) zinaendelea kutumika kama sehemu muhimu za AU katika suala la kuunganishwa na raia wake. Ushirikiano wa kikanda wa Afrika ni muhimu katika kuendeleza malengo yake ya maendeleo, kwani hurahisisha uundaji na utekelezaji wa suluhisho za kikanda kwa changamoto za kitaifa kwa kukabiliana na vikwazo vya rasilimali chache na uwezo mdogo katika ngazi ya kitaifa. Mradi wa Pan-African unakusudiwa kuendeleza ushirikiano wa kikanda kupitia RECs, ambazo hufanya kazi kama vizuizi muhimu katika mchakato huu. Ushiriki wa asasi za kiraia za Kiafrika ni muhimu katika kuimarisha RECs, kwani zinahakikisha ushiriki mkubwa na kuidhinishwa kwa raia katika mikakati yao, huku zikihakikisha kuwa mikakati hii ni wakilishi na yenye ufanisi katika kukidhi matarajio ya watu wa Afrika.

## Demokrasia na nafasi za kiraia - vikwazo hatari

Kuna changamoto changamano katika kuanzisha demokrasia ya kweli barani Afrika.

Mataifa mengi ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara yalianzishwa kwa misingi ya ukoloni, mfumo wa unyonyaji, hali iliyosababisha miundo dhaifu ya kusaidia kukuza demokrasia huria. Mazingira ya kisiasa yametatizwa zaidi na migawanyiko ya kidini na kikabila, hali ambayo wakati mwingine imeundwa na watu ili kunufaisha kundi finyu la viongozi wa kisiasa. Katika jitihada za kuonekana kuwa za kidemokrasia na kupata uhalali wa kimataifa, serikali nyingi za utawala wa kimabavu na nusu-mabavu barani Afrika zimechukua sura za kidemokrasia. Serikali hizi zinafanya chaguzi, ambazo mara kwa mara hubadilishwa,

pamoja na hayo, zinadai kufuata mgao wa mamlaka na ukomo wa muda wa mihula ya urais, ingawa mara nyingi huunda 'mapinduzi ya kikatiba' ili kukwepa mipaka hii ya muda wa mihula ya rais.

Kunayo hali ya kuzorota kwa nafasi za kiraia duniani, Afrika ikiwemo pia. Watetezi wa haki za binadamu na wanaharakati wa mashirika ya kiraia wanakabiliwa na hatari kubwa, ikiwa ni pamoja na kufungwa au hata kupoteza maisha. Data ya Civicus Monitor inaonyesha kuwa 28% ya watu duniani wanapitia viwango vya juu vya ukandamizaji, huku waandishi wa habari pia wakikumbana na unyanyasaji na mashambulizi ya kimwili, hasa wanaporipoti maandamano.[19] Licha ya changamoto hizi, umma kuunga mkono hatua za kidemokrasia bado upo imara barani Afrika, kama inavyothibitishwa na tafiti za Afrobarometer: katika utafiti wake wa kina katika nchi 34 za Afrika, taasisi hiyo imefichua kuwa, 68%, ya watu wanaonyesha upendeleo wa demokrasia kuliko aina nyingine yoyote ya utawala.[20]

## Uhamiaji - shinikizo lililochanganywa na fursa

Ukosefu wa utulivu wa kisiasa, tofauti za kiuchumi na masuala ya mazingira barani Afrika yamezidisha mzozo wa uhamiaji na ongezeko la wakimbizi, hali ambayo imelifanya hili kuwa suala kuu la kibinadamu. Hata hivyo, AU inasema Afŕika inachangia asilimia 14% ya idadi ya wahamiaji duniani, ikilinganishwa kwa mfano, 41% kutoka Asia na 24% kutoka Ulaya.[21] Ingawa tunatambua athari kubwa za kibinadamu za uhamiaji, pia kuna upande mzuri na manufaa ya uhamiaji ndani na kutoka Afrika. Hii inaangazia uhamishaji wa ujuzi ndani ya Afrika ambao unasaidia katika ukuaji, na fedha zinazotumwa kutoka nje zinazokuza uwekezaji barani Afrika na vile vile misaada kwa ajili ya harakati za kibinadamu na maendeleo. Mtiririko wa kutuma pesa barani Afrika uliongezeka maradufu katika mwongo uliopita, na kufikia bilioni $100 mwaka wa 2022, na kupita fedha zilizopokelewa kupitia programu za Usaidizi Rasmi wa Maendeleo (ODA) na Uwekezaji wa Moja kwa Moja wa Kigeni (FDI).[22]

Suala la uhamaji limejikita sana katika haki za binadamu na linaunganishwa na Itifaki ya AU ya Mwendo Huru wa Watu Barani Afrika. Itifaki hii inatetea haki za watu binafsi kuhama kwa uhuru katika bara zima, huku ikisisitiza umuhimu wa njia halali na salama za uhamiaji katika kudumisha utu na haki za binadamu. Kwa kuwezesha njia hizi, itifaki inalenga sio tu kupunguza hatari za uhamiaji usio wa kawaida lakini pia kukuza michango chanya na mizuri ya uhamiaji kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi asili na wenyeji katika bara la Afrika.

## Haki za kidijitali

Mazingira ya kidijitali barani Afrika yanakua. Idadi ya watumiaji wa kipekee wanaotumia huduma za simu inatarajiwa kuongezeka kutoka milioni 489 (43%) mwaka wa 2022 hadi kufikia milioni 692 (50%) ifikapo 2030.[23] Afrika ina idadi kubwa zaidi ya watu wenye umri mchanga duniani, ikiwa na asilimia 70 ya wakazi wa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara chini wakiwa na miaka 30.[24] Hii ina uwezo mkubwa wa Afrika kuziba ukosefu wa usawa na kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu. Uwezo wa kiuchumi wa bara unaweza kupanuka kwa kiasi kikubwa, mradi tu idadi ya vijana inayoongezeka ina vifaa na fursa muhimu.

Vijana wa Afrika wametumia fursa ya intaneti na mitandao ya kijamii kujihusisha na siasa. Hata hivyo, bado kuna wasiwasi mkubwa kuhusu urudufishaji wa ukosefu wa usawa wa nje ya mtandao kupitia sheria na kanuni za kuwarudisha watu nyuma; kuna vizuizi vinavyoendelea kwa matumizi ya mtandao wa simu katika nchi kama vile Benin, Chad na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ambapo viwango vya kupenya kwa mtandao wa simu za mkononi viko chini ya 15%. Masuala kama vile ulinzi wa data, faragha, usalama, unyanyasaji mtandaoni, mashambulizi ya mitandao, kuzimwa kwa mitandao kunakofadhiliwa na serikali na kupanua mgawanyiko wa jinsia wa kidijitali unaohitaji uangalizi wa haraka. Kuenea kwa unyanyasaji mtandaoni, hasa dhidi ya wanawake na wasichana, kunaakisi na kukuza masuala ya kijamii, huku 38% ya wanawake duniani wakiripoti unyanyasaji mtandaoni.[25] Hii inaangazia hitaji la dharura la kushughulikia maswala haya ya usalama wa kidijitali ili kuunda mazingira jumuishi na salama mtandaoni.

# Huduma za umma kitovu cha ukosefu wa usawa

Mnamo 2022, serikali za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara zilitumia wastani wa 3.22% ya Pato lao la Taifa kwenye elimu, hii inaonyesha kupungua kwa kiasi cha awali kutoka kiwango cha 2013 (3.69%).[26] Hali hii imechangia kuzorota kwa matokeo ya elimu, kama inavyothibitishwa na ongezeko la asilimia ya vijana wasiojishughulisha na elimu, ajira au mafunzo. Nchini Mali, takwimu hizi ziliongezeka kutoka 13.47% ya vijana mwaka 2010 hadi 30.86% mwaka 2020, huku nchini Zimbabwe, takwimu zikiongezeka kutoka 17.26% mwaka 2011 hadi 30.43% mwaka 2021, hali hii inaonyesha kurudi nyuma kwa maendeleo na ushiriki wa vijana.[27] Mapungufu katika mifumo ya elimu ya Afrika, pamoja na changamoto katika upatikanaji wa huduma za afya na huduma za usambazaji wa maji safi, yanadhihirisha kushindwa kushughulikia ukosefu wa usawa na faida za kidemokrasia zilizoahidiwa. Upungufu huu, unaodhihirika miongo sita baada ya nchi nyingi za Kiafrika kurejea katika utawala wa kikatiba, unajumuisha mapungufu katika hifadhi ya jamii, ajira, mgao wa faida za ukuaji wa uchumi wenye haki, na utawala wa sheria, na hivyo basi kudhoofisha imani ya wananchi katika mchakato wa kidemokrasia. Ni muhimu kukabiliana na mapungufu haya ya kiutawala na serikali kwa kina, kwa kukita mizizi ya siasa, uchumi na jamii. Kufanya hivyo ni muhimu kwa ajili ya kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDGs), maono yaliyoainishwa katika Ajenda ya AU ya 2063, na malengo ya Eneo la Biashara Huria la Bara la Afrika. Kwa kushughulikia changamoto hizi, Afrika inaweza kuibuka mstari wa mbele katika maendeleo ya kimataifa.



Patience (36) anatafakari jinsi ya kubadilisha maisha yake ili kukabiliana na mgogoro wa gharama za maisha zinazopanda kila siku. Patience ni muuguzi katika Hospitali ya Mafunzo ya Korle Bu nchini Ghana na hawezi kuhudumia watu wanaomtegemea kwa mshahara wake wa kila mwezi. *Picha ni kwa hisani ya: Ernest Ankomah / Oxfam*

# 3.3 UDHAIFU NA MIGOGORO INAYODHOOFISHA MAENDELEO

Afrika ni makao ya baadhi ya maeneo yenye njaa nyingi sana duniani; bara la Afrika ina 54% ya jumla ya idadi ya watu walio katika hali mbaya au mbaya zaidi kuathiriwa na njaa, hii ni kulingana na Ripoti ya Kimataifa ya 2020 kuhusu Migogoro ya Chakula.[28] Sababu kuu za njaa hii kali ni pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa, migogoro na ukosefu wa uwekezaji wa umma katika kilimo, jambo ambalo linazidisha uhaba wa chakula katika bara zima.

## Migogoro

Mwanzoni mwa 2023, 13% ya nchi za Afrika zilikumbwa na mapinduzi katika miaka miwili iliyopita – ongezeko la mara sita kutoka miaka minne ya awali.

Utafiti unaonyesha kuwa tangu mwaka wa 1950, kumekuwa na angalau jaribio moja la mapinduzi ya serikali katika mataifa 45 kati ya 54 barani Afrika.[29] Hasa, nchi katika eneo la Sahel, Afrika ya Kati na Pembe ya Afrika zimepitia changamoto kubwa zinazotokana na migogoro ya kisiasa, utawala dhaifu na uwepo wa watendaji wasio wa serikali au wasiounga serikali mkono. Mivutano ya kisiasa inayoendelea, vita na migogoro barani Afrika imesababisha athari mbaya kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya bara hilo, na kusababisha mamilioni ya watu kuyahama makazi yao. Katika kukabiliana na hali hiyo, AU imetekeleza kanuni na viwango mbalimbali vinavyolenga kukuza ushirikiano wa pande nyingi, utawala, demokrasia na haki za binadamu katika kanda nzima. Kipengele cha msingi cha mfumo huu ni Mweleko wa Utawala wa Afrika, ulioanzishwa mwaka wa 2011 ili kuimarisha uratibu na ushirikiano kati ya vyombo na taasisi za bara na kanda, kwa kulenga utawala, demokrasia na masuala ya haki za binadamu.

Kushughulikia changamoto ya mizozo barani Afrika na kupambana na kutojali kukohusisishwa na hali hii, kutahitaji juhudi zilizoratibiwa katika ngazi za kitaifa, kikanda na kimataifa. Katika kukabiliana na ongezeko la ukosefu wa utulivu wa kisiasa na migogoro barani Afrika, hasa katika kanda kama vile Sahel, Afrika ya Kati na Pembe ya Afrika, OiA inasisitiza haja ya mbinu zinazojali migogoro katika mikakati yake ya kuingilia kati. Tukizingatia mwingiliano changamano kati ya mivutano ya kisiasa, utawala dhaifu na ushawishi wa watendaji wasio wa serikali, masuala nyeti katika migogoro lazima yajumuishwe katika shughuli za kibinadamu na katika uundaji na utekelezaji wa programu. Mbinu hii inahakikisha kwamba mipango haizidishi migogoro bila kukusudia bali inachangia katika ukuzaji wa amani na maendeleo endelevu.

## Athari za Mabadiliko ya Hali ya Hewa

Licha ya kuchangia kwa kiwango kidogo katika mgogoro wa hali ya hewa unaosababishwa na binadamu, Bara la Afrika ndilo bara linaloathiriwa zaidi na mabadiliko ya hali ya hewa na linabeba hatari za kimfumo. Mgogoro wa hali ya hewa ni jambo la pande nyingi, lililo na hali inayoongeza athari kwa mazingira magumu, hali inayowapitisha watu kwa mazingira magumu na athari kwa watu, hasa kwa wanawake.

Wakati wa kuchapishwa kwa mkakati huu, inaonekana wazi kuwa kuna uwezekano mkubwa kwamba lengo la Makubaliano ya Paris la kupunguza ongezeko la joto duniani hadi nyuzijoto 1.5 halitaafikiwa. Kwa hivyo, mabadiliko ya kimataifa ya sekta ya nishati ni muhimu ili kupunguza ongezeko la halijoto na kudhibiti uharibifu unaohusika na ongezeko hilo kadiri inavyowezekana. Mabadiliko katika nishati kwa upande mmoja, na matumizi ya rasilimali kwa upande mwingine, yanawasilisha mandhari changamano ya athari kwa maendeleo endelevu ya Afrika. Huku bara likikabiliana na mahitaji yake ya nishati yanayoongezeka, mabadiliko kuelekea vyanzo vya nishati safi na vinavyoweza kutumika tena ni muhimu ili kupunguza athari za

nishati kwa mazingira na kushughulikia mabadiliko ya hali ya hewa. Mpito huu unatoa fursa na changamoto. Afrika ina vyanzo vingi vya nishati mbadala na safi, vikiwemo nishati ya jua, umeme unaotokana na maji na upepo. Afrika pia ni makao ya akiba kubwa ya madini muhimu kwa upana ili kutoa suluhisho za nishati safi; Afrika ina zaidi ya 40% ya akiba ya ulimwengu ya Kobalti, manganese na platinamu, ambayo ni muhimu kwa utengenezaji wa betri na teknolojia ya nishati ya haidrojeni. Hii inatoa fursa muhimu ya kuimarisha usalama wa nishati na kupunguza utoaji wa gesi chafu. Hata hivyo, kutambua mabadiliko haya kutahitaji uwekezaji mkubwa katika miundombinu na teknolojia. Ni muhimu kuwepo na usawa katika mabadiliko haya ya nishati ili kuboresha matumizi ya rasilimali. Hii ni muhimu kwa Afrika ili kutimiza ajenda yake ya ukuaji wa teknolojia inayozingatia mazingira na hali yake ya hewa na tabianchi, hali itakayohakikisha upatikanaji wa haki ya nishati safi na kuzuia umaskini wa nishati miongoni mwa jamii zilizotengwa.

## Ukosefu wa uwekezaji katika kilimo

Licha ya jukumu muhimu ambalo kilimo kinachukua katika mfumo wa kiuchumi na kijamii wa Afrika, uwekezaji duni wa muda mrefu umeendelea, ukizuia kwa kiasi kikubwa juhudi za kupunguza njaa na kukuza maendeleo endelevu. Baada ya utatizaji wa uchumi wa dunia na katika mgogoro wa hali ya hewa unaoongezeka, haja ya kuongeza uwekezaji wa kilimo haijawahi kuwa dhahiri zaidi kama ilivyo sasa. Takwimu za hivi majuzi zinaonyesha hali ya kutisha: serikali nyingi za Afrika (48 kati ya 54) zimeripotiwa kutenga wastani mdogo wa 3.8% ya bajeti zao zote kwa sekta ya kilimo katika mwaka wa 2021,[30] na karibu robo tatu ya serikali za Afrika zimepunguza bajeti zao za kilimo. Viwango hivi havifikii lengo lililowekwa la Azimio la Malabo la 10% ya lengo la uwekezaji lakini pia linatofautiana kwa kiasi kikubwa na matumizi makubwa yasiyo na uwiano kwenye silaha za kijeshi, ambayo ni 6.4%.[31]

Athari za uwekezaji huu duni ni kubwa, haswa katika bara ambalo theluthi moja ya watu wake wanakabiliwa na utapiamlo na 30% ya watoto wamedumaa kwa sababu ya utapiamlo.[32]



Ouahigouya commune - Burkina Faso. Aguiratou Ouedraogo ni mkulima. Ana umri wa miaka 39, mama wa watoto 7. Anachota maji kisimani kumwagilia mazao yake ya kuuza sokoni, akisaidiwa na mkulima mwenzake wa kike ambaye anashiriki naye ploti hiyo ndogo ili kufanya kilimo. *Picha ni kwa hisani ya : Samuel Turpin/ Oxfam*

# 3.4 UKIUKAJI WA HAKI ZA WANAWAKE NA UDHALIMU WA KIJINSIA UNAENDELEA KUZUIA MAENDELEO

Kanuni za kitamaduni hutia mifumo wa ubabedume nguvu, mifumo ambayo huwapa wanaume upendeleo juu ya wanawake. Mifumo ya sasa ya kiuchumi, ambayo ni ya mfumo wa ubabedume, uliberali mamboleo na ya unyanyasaji kiasili, inategemea utunzaji wa riziki, wakati huo huo inaidharau, inaidhoofisha na kukataa hata kutambua huduma za ulinzi kama kazi. Mifumo hii pia inatanguliza faida ya muda mfupi dhidi ya gharama ya hasara ya muda mrefu (mazingira, utunzaji, ustawi), kama ilivyoangaziwa na janga la COVID-19. Wanawake wengi walioajiriwa barani Afrika wanafanya kazi katika sekta isiyo rasmi, ambayo haihesabiwi kama sehemu ya Pato la Taifa na ina sifa za ukosefu wa usalama, ukosefu wa usawa wa mishahara na utambuzi duni wa mchango wa kifedha unaotolewa kwa uchumi.

Kushughulikia ukosefu huu wa usawa wa kimuundo ni muhimu ili kuhakikisha haki sawa za wanawake na ushiriki wao kamili katika jamii. Kutambua haki za wanawake hakuhitaji ulinzi wa kisheria pekee bali pia kunahitaji mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi na kijamii ambayo kwa sasa inawatenga au kuwaweka pembeni wanawake. Kupitia mabadiliko ya sera za makusudi na mifumo inayoshughulikia jinsia, utambuzi wa haki sawa za wanawake utakuwa msingi na wenye juhudi pana za kuelekea haki za kijamii na kiuchumi.

Licha ya baadhi ya mataifa ya Afrika kuwa na haki za kijinsia zenye kuleta maendeleo kulingana na sheria, mara nyingi ukweli mashinani unadhihirisha unyanyasaji wa kijinsia ulioenea na mila zenye madhara. Wanawake wengi sana wa Kiafrika wamenyimwa uwezo wa kusimamia maisha yao wenyewe na kushiriki katika serikali, kwa kuwa wanakosa uwezo wa kufikia mahitaji ya kimsingi kama vile elimu bora na huduma za afya, na wana hadhi ya chini ya kijamii. Uwezo wa wasichana na vijana wa kike kufikia, kupata, kubaki na kumaliza shule bado ni wa wasiwasi mkubwa barani Afrika. Takwimu kutoka UNESCO (2019) zinaonyesha kuwa wasichana milioni 52 hawako shuleni barani Afrika, na wasichana milioni nne hawajawahi kuingia darasani, ikilinganishwa na wavulana milioni mbili.[33] Hii ni changamoto kubwa kwa Afrika na kuna uwezekano wa changamoto hii kuathiri uafikiaji wa malengo ya Ajenda ya 2063 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Kuna dharura ya haraka ya kuziba pengo hili. Matokeo ya utafiti wa Afrobarometer wa mwaka wa 2023 yanaangazia hali ngumu ya unyanyasaji wa kijinsia barani Afrika na changamoto nyingi za kushughulikia unyanyasaji huo. Utafiti unaonyesha kuwa ingawa sehemu kubwa ya watu wanatambua tatizo hilo, mitazamo iliyokita mizizi inawezesha kuendelea kwake, na ujenzi wa mazingira salama kwa wasichana na wanawake kutahitaji kampeni za elimu na uhamasishaji pamoja na mifumo madhubuti ya kisheria na utekelezaji wa sheria unaoendelezwa na watu waliopokea mafunzo yafaayo'.[34] Utambuzi huu wa watu unatoa fursa nzuri ya kushirikiana na watu wa Afrika, wakiwemo wanaume na wavulana ili kukomesha unyanyasaji wa kijinsia.

Wanawake hawajateseka wakiwa wamenyamaza. Wamekuwa wakifanya kazi kwa bidii ili kupata mifumo bora zaidi ya kujilinda, ikiwa ni pamoja na kutetea kwa mafanikio mikataba ya kimataifa na kuimarishwa kwa mikataba hiyo katika bara nzima. Mashirika ya kiraia yaliyopangwa kikanda na kote barani Afrika yanatoa uwezo mkubwa na unaoongezeka juu ya watendaji wa kisiasa na watu binafsi. Katika ngazi ya kisiasa, kwenye bara zima, AU ni kichocheo kizuri na kifaacho cha kubadili kanuni za kijinsia, na Itifaki ya Maputo kwa Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu, iliyopitishwa na Marais wa Nchi na Serikali za Afrika mwaka wa 2003 na kuanza kutumika mwaka wa 2005 ni hati muhimu ya kisera.

# 4.0

# NGUVU ZA KULETA MABADILIKO (UCHAMBUZI WA UONGOZI)

Mabadiliko endelevu yatatokea barani Afrika wakati taasisi na watu walio na mamlaka watabadilika ili kuleta ushirikishaji na ujumuishaji. Sehemu hii inaeleza jinsi OiA itaingiliana na wamiliki wakuu wa uongozi katika mfumo wa kimataifa, na wenye mamlaka katika viwango mbalimbali vinavyohusiana na kila moja ya nguzo tano za mkakati huu.

## Washirika wa kimataifa

***Serikali za wafadhili, wafadhili wa nchi kwa nchi, INGOs na mashirika ya Umoja wa Mataifa*** ndio wamiliki wakuu katika mfumo wa kimataifa, na pia ndio watoa huduma rasmi wakubwa wa mtaji na usaidizi wa maendeleo katika sehemu ya Kaskazini mwa Ilimwengu. Washirika hawa wanakuza na kudumisha hali iliyopo ya biashara kimataifa, misaada na maendeleo. Mashirika na serikali za Kaskazini mwa Ulimwengu, wafadhili mbadala na mashirika ya kimataifa hudhibiti ajenda, huamua mahali ambapo fedha na biashara hutiririka, na kuelekeza mazungumzo kuhusu mustakabali wa Nchi za Kaskazini ulimwengu. *OiA pamoja na washirika wake itawawajibisha washirika wa kimataifa kuhusu matumizi ya nguvu hizi kubwa, na itapinga sera zao, vitendo na kutochukua hatua kunakoendeleza ukosefu wa usawa na maendeleo duni barani Afrika.*

## Uchumi wenye haki

***Serikali zinazokopesha nchi nyingine na taasisi za fedha za kimataifa (IFIs)*** – Serikali zinazokopesha nchi pesa na IFIs, ambazo nyingi ni mabaki ya enzi ya ukoloni, zina ushawishi mkubwa juu ya mfumo wa fedha wa kimataifa, kuunda ajenda ya maendeleo ya kimataifa na kudhibiti misaada na ufadhili wa mikopo kutoka Nchi za Kaskazini mwa Ulimwenguni. Vitendo na sera zao zina athari kubwa kwa uchumi wa nchi nyingi za ulimwenguni[35]. Ili kurekebisha ukosefu wa usawa wa kihistoria na kuhakikisha kushughulikiwa kwa usawa, mojawapo ya vipaumbele vya OiA itakuwa kutetea mageuzi makubwa ya IFIs. Mabadiliko haya yatalenga kuhakikisha kuwa taasisi hizi zinahudumia Nchi Zinazoendelea kwa ufanisi kama zinavyofanya nchi za Kaskazini mwa Ulimwengu. *Serikali zinazokopesha nchi na IFIs zitakuwa vipaumbele muhimu kwa OiA na washirika wake.*

***Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda[36] na Umoja wa Afrika*** – Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs) na AU zina jukumu muhimu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi barani Afrika kupitia mifumo na maamuzi yao ya kimkakati. Mashirika haya yanaunda sera na mipango inayoathiri mwelekeo wa uchumi wa bara hili, yakiwa na lengo lililobainishwa la ushirikiano wa kikanda na maendeleo endelevu. OiA itaendelea kushirikiana na RECs na AU, kuleta matokeo ya utafiti na mitazamo ya jamii iliyoathirika katika michakato yao. Ushiriki huu ni muhimu ili kuhakikisha kwamba sauti za watu zinasikika na mahitaji yao yanashughulikiwa katika mifumo na mipango ya kimkakati ya mashirika haya. OiA pia ina jukumu muhimu katika kushikilia mashirika haya ya kikanda kuwajibika juu ya ahadi zao, hali itakayohakikisha kuwa maamuzi yanatekelezwa ipasavyo na kunufaisha watu wanaokusudiwa kuwasaidiwa. Kushirikiana na kushawishi RECs na AU ili kuweka kipaumbele na kuchukua hatua juu ya maendeleo ya kiuchumi yenye usawa na ukuaji endelevu ni muhimu. *RECs na AU watakuwa washirika na walengwa muhimu kwa OiA na washirika wake, na hivyo kuhitaji ushirikiano endelevu ili kushawishi sera na kuufanya uongozi kuwajibikia maamuzi yao.*

***Serikali za kitaifa na za mitaa*** – Ingawa serikali za kitaifa na za mitaa zinatoa mamlaka fulani kwa serikali kuu zaidi katika suala la uundaji wa sera, serikali hizi zina jukumu la kuhakikishia raia wake haki za kiuchumi. Ili kuhakikisha mgao sawa wa mali na kupunguza ukosefu wa usawa, kuna haja kubwa ya kutetea mifumo ya kodi yenye maendeleo ambayo inahakikisha kwamba watu matajiri na mashirika makubwa yanachangia mgao wa haki katika mapato ya taifa. *OiA itafanya kazi ili kuhakikisha kuwa sauti za watu zinazingatiwa katika kuunda sera ya kitaifa, kukuza ushirikiano na kuimarisha uwajibikaji katika utekelezaji wa sera.*

***Mashirika*** – Serikali za kitaifa zinasalia kuwa wamiliki wakuu katika suala la utawala. Imedhihirika kwamba demokrasia kote barani Afrika imerudi nyuma. *OiA itatoa changamoto kwa mashirika kuhakikisha ukuaji endelevu na ugawaji wa haki wa manufaa yanayotokana na ukuaji huo.*

## Utawala unaowajibika na jumuishi

***Serikali za kitaifa na za mitaa*** – National governments remain the key power holders when it comes to governance. Significant democratic backsliding has taken place across Africa. *OiA italenga kujenga michakato ya kidemokrasia na vuguvugu thabiti linalowafanya viongozi kuwajibika.*

***Mahakama na mifumo ya kisheria ya maeneo*** – Mahakama zinazojitegemea zinatakiwa kufuatilia mamlaka ya utawala na kuhakikisha haki za kimsingi za kujieleza, kutoa maoni, kushiriki na kushirikiana, ingawa uwezo wao katika nchi za Afrika hutofautiana sana. *OiA inaweza kusaidia harakati za watu kupigania mahakama huru.*

***Mashirika ya kiraia na harakati za vijana na mashinani*** – Mashirika ya kiraia na harakati nyingine zimepata nguvu kupitia ushirikishwaji thabiti, wakati mwingine, kumekuwa na mivutano baina ya raia na serikali. *Kuhakikisha nafasi wazi za kiraia kwa makundi haya ni muhimu kwa ajili ya kufikia utawala wenye uwajibikaji na kuhakikisha kuwa vijana, wanawake na makundi mengine yaliyo hatarini, na vyombo vya habari wanashiriki katika harakati za kiraia.*

## Haki za mabadiliko ya hali ya hewa

***Umoja wa Mataifa*** – Katika ngazi ya kimataifa, Umoja wa Mataifa una ushawishi mkubwa katika haki za mabadiliko ya hali ya hewa. Ikiwa Umoja wa Mataifa utashindwa kuendeleza haki za hali ya hewa, basi kwa pamoja itashindwa kulinda haki za binadamu na haki za vizazi vijavyo. *Kwa OiA na washirika wake, Umoja wa Mataifa na washiriki wake wengine wanatoa fursa muhimu za kushawishi na kutetea mabadiliko.*

***Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kiuchumi za Kikanda (RECs)*** – AU na RECs zinaendesha mwitikio wa bara la Afrika kwa mabadiliko ya hali ya hewa. Kupitishwa kwa Azimio la Nairobi kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Wito wa Kuchukua Hatua[37] na Viongozi wa Afrika mnamo Septemba 2023 kunaashiria azimio la pamoja la kushughulikia mgogoro wa mabadiliko ya hali ya hewa. Hata hivyo, mashirika ya kikanda na bara lazima yatoe suluhu za mbinu zinazozingatia watu zaidi kipaumbele dhidi ya zile zinazoendeshwa na soko, hali

inayohakikisha haki za hali ya hewa na maendeleo endelevu. *Kwa OiA, kushirikiana na AU na RECs ni muhimu ili kukuza utetezi wake wa haki ya hali ya hewa, hali itakayohakikisha kwamba sera na hatua zinazoidhinishwa katika ngazi za bara na kikanda zinapatana na mahitaji ya mashinani na kuchangia kikamilifu katika SDGs.*

***Serikali za kitaifa*** – Serikali za kitaifa zinashikilia mamlaka ya kuhakikisha kuwa mpito kuelekea uchumi safi unafanywa kwa njia isiyomwacha mtu yeyote nyuma. Pia wana mamlaka ya kudhibiti mashirika kufikia mienendo inayolinda mazingira. *Serikali za kitaifa zinasalia kuwa mshirika na walengwa wakuu katika kazi ya ushawishi ya OiA.*

***Mashirika*** – Mashirika yana mamlaka juu ya serikali na watu na huchangia katika mgogoro wa hali ya hewa wakati yanapotoa gesi chafu. *Mashirika ni walengwa muhimu katika utetezi wa OiA.*

***Mashirika ya Kimataifa Yasiyo ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Serikali (INGOs na NGOs)*** – Mashirika haya yanafanya kazi ya kujenga mamlaka ya kisiasa na ushawishi ili yaweze kushinikiza serikali na sekta ya kibinafsi na kuwawajibisha watendaji wenye nguvu. *INGOs na NGOs ni washirika muhimu sana wa OiA.*

## Haki za kijinsia

***Miundo ya mfumo wa ubabedume*** – Mamlaka kwa kawaida huwekwa chini ya viongozi wa kiume, wa kidini, wa kijamii au wa kitamaduni, na hupendelea wanaume. Kuhamisha mamlaka haya hakuwezi kupatikana kupitia sheria pekee; pia ni muhimu kubadili mitazamo na kanuni za kijamii. *OiA na washirika wanahitaji kuzingatia kubadilisha mitazamo na kanuni hizi. Wanaume na wavulana wanaweza kuwa washirika muhimu katika kuleta mabadiliko haya.*

***Umoja wa Afrika*** – Vyombo na mashirika ya AU ni wahusika wakuu katika bara zima katika kukuza na kudumisha Itifaki ya Maputo katika nchi za Afrika. Kwa kuweka Kurugenzi ya Wanawake, Jinsia na Vijana moja kwa moja chini ya uongozi wa Naibu Mwenyekiti, Tume ya AU inasisitiza kipaumbele kwa masuala ya kijinsia katika ajenda ya shirika hilo. *Huku AU inapoendelea kukuza ushawishi wake, hili ni shabaha muhimu na vile vile mshirika wa OiA, na inaweza kuunda mazingira sahihi ya ushiriki na ya mabadiliko kutokea.*

***Serikali za kitaifa*** – Serikali za kitaifa zina ushawishi mkubwa kwa watu, mifumo ya kitaasisi na nafasi za kiraia katika maeneo yao ya utawala. Serikali hizo ni muhimu katika kuunda sera zinazotawala mahusiano ya kijinsia na katika kubomoa miundo ya mfumo wa ubabedume inayopendelea wanaume. Ushiriki huu ni muhimu kwa ajili ya kujenga mazingira wezeshi ambapo wanawake na wasichana wanawezeshwa kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za kijamii. Serikali za kitaifa pia zina jukumu madhubuti katika kutenga rasilimali na kuendeleza programu zinazounga mkono ujumuishaji wa kijinsia katika sekta mbalimbali, hali inayozifanya serikali hizi kuwa washirika wasioepukika katika kuendeleza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake. *Kwa kushirikiana na serikali za kitaifa, OiA itawezesha kupitishwa na kutekelezwa kwa sera zinazoendeleza usawa wa masuala ya kijinisia, ikiwa ni pamoja na uundaji na matumizi ya mikataba ya kimataifa kama vile Itifaki ya Maputo.*

***Mashirika ya kiraia*** – Mashirika ya kiraia ya Kikanda na ya bara zima la Afrika yana jukumu muhimu katika kutetea utawala bora, haki za binadamu na haki za wanawake. Makundi haya yana ushawishi mkubwa kwa watendaji wa kisiasa na watu binafsi, kwa kuwa yanapinga kanuni za mfumo wa ubabedume na kutetea mabadiliko ya kimfumo. Pia ni muhimu katika kuwajibisha serikali na kuhakikisha kwamba haki za kijinsia ni muhimu katika utungaji sera na utekelezaji wa sera. Miungano yao ya kimsingi na uelewa wa kina wa muktadha wa eneo husika huwafanya kuwa wahusika wakuu katika utetezi wa mageuzi yanayozingatia jinsia na katika kuhamasisha jamii kudai na kushughulikia wanawake na wasichana kupata usawa. *Kupitia ushirikiano na mashirika ya kiraia, OiA inalenga kukuza sauti za wanawake wa Afrika na kuhakikisha ushiriki wao kikamilifu katika kuunda jamii yenye haki na jumuishi.*

## Hatua ya usaidizi wa kibinadamu

***Mashirika ya kimataifa ya wafadhili na INGOs*** – Wafadhili wa serikali za Kaskazini mwa Ulimwengu, mashirika ya Umoja wa Mataifa na mashirika ya kimataifa yasiyo ya serikali (INGOs) wanashikilia mamlaka makubwa kupitia rasilimali wanazodhibiti. Msukumo kuelekea umiliki wa jamii ni muhimu katika kugawana mamlaka, na OiA lazima iamue kuongoza katika mabadiliko haya. *Kwa kushawishi wahusika hawa kwa ajili ya kufanya maamuzi na ugawaji wa rasilimali unaofaa jamii zaidi, OiA inalenga kuhakikisha kuwa mwitikio kwa masuala ya kibinadamu yanakidhi mahitaji ya jamii zilizoathirika, na kwamba yanawiana na kanuni za usawa na haki pamoja na ahadi zinazotolewa na Oxfam kama vile; The Grand Bargain,[38] Mkataba wa Mabadiliko[39] na Ahadi ya Mabadiliko.[40]*

***Serikali za kitaifa na za mitaa*** – Serikali za kitaifa na za mitaa wana jukumu la mwisho kwa wale walioathiriwa na maafa; wanaweza kufikia pamoja na kudhibiti eneo lililoathiriwa. *OiA itahitaji kuonyesha mshikamano kwa kuwezesha ufikiaji wa rasilimali na vile vile kulenga serikali hizi ili kuhakikisha ufikiaji wa jamii zilizoathiriwa.*

***Jamii na Uongozi wa jamii*** – Wazee na viongozi wa jamii, au wale wanaosimamia miktadha ya eneo, wanashikilia mamlaka juu ya wakazi wa eneo hilo wakati wa hatua za usambazaji wa usaidizi wa kibinadamu. Kwa kuwezesha uongozi wa eneo na kuweka kipaumbele kwa mahitaji na sauti za watu walio hatarini zaidi, hasa wakimbizi, watu waliokimbia makazi yao, na wanawake na wasichana, OiA inalenga kukuza matokeo ya usawa na endelevu ya kibinadamu. Mtazamo huu unaozingatia jamii unahakikisha kwamba hatua za kibinadamu zinaongozwa na kanuni za haki na zina umuhimu kwa jamii, na hivyo kusababisha uingiliaji kati wa kibinadamu wenye ufanisi zaidi na wenye matokeo. *Mtazamo wa ufeministi wa Oxfam utakuwa kichocheo kikuu katika kubadilisha mamlaka ya nafasi ya uongozi wa jamii au wa eneo.*



Asha Sode, Masu Wache, Fatuma Adan wanachama wa kikundi cha wanawake cha Uye katika Kaunti ya Marsabit, Kenya, washiriki katika mradi wa mwitikio wa uzalishaji wa chakula unaofadhiliwa na NORAD, wakiwa katika mkutano wa Akiba na Mikopo wa Kijiji, mafunzo kutoka kwa PACIDA, shirika la washirika wa OXFAM. *Picha ni kwa hisani ya: Misheck Kamau/Oxfam*

# 5.0

# MALENGO YA OXFAM BARANI AFRIKA

## Maono yetu

Afrika iliyo na usawa.

## Dhamira yetu

Kupambana na ukosefu wa usawa na kubomoa miundo ya mamlaka kwa kuwaweka wanawake, vijana, Jamii Wenyeji na makundi mengine yaliyo hatarini kwenye mstari wa mbele na kujenga mustakabali ulio na usawa kwa Afrika kama sehemu ya ulimwengu ulio na usawa zaidi.

Tunakubaliana na kujisajili kutumia maadili ya Oxfam duniani kote, na kujumuisha maadili ya uhusiano na kutegemeana.

## Maadili yetu

- **Usawa:** Tunaamini kila mtu ana haki ya kutendewa haki na kuwa na haki na fursa sawa.
- **Uwezeshaji:** Tunakubali na kutafuta kupanua uwezo wa watu katika maisha yao na maamuzi yanayowaathiri.
- **Mshikamano:** Tunaungana mikono, kusaidia na kushirikiana kuvuka mipaka katika kufanya kazi kuelekea ulimwengu wa haki na wenye uendelevu.
- **Ujumuishaji:** Tunakumbatia utofauti na tofauti, na kuthamini mitazamo na michango ya watu wote na jamii katika vita vyao dhidi ya umaskini na ukosefu wa haki.
- **Uwajibikaji:** Tunawajibikia vitendo vyetu na ukosefu wetu wa kutochukua hatua, na kuwajibika kwa watu tunaofanya nao kazi
- **Ujasiri:** Tunasema ukweli kwa mamlaka na kutenda kwa imani kuhusu haki ya yale tunayopigania .
- ***Ubuntu* ('Nipo kwa sababu tupo'):** Tunategemeana kabisa - tunashindwa au tunashinda kwa pamoja.

## Kusudi letu

Kiongozi **anayefikiria** - sisi ni jukwaa la kujifunza na kubadilishana maarifa, kiongozi katika uvumbuzi, na kiunganisha cha kujifunza.

Mratibu **na mwezeshaji** - tunaleta pamoja mawazo tofauti na kuunda umoja kati ya wale wenye malengo sawa.

Mshiriki **na amplifaya** - tunakuza ushirikiano na kuinua sauti za watu wanaoishi katika eneo na kukuza sauti zao mbali na eneo lao.

**Mwezeshaji** - sisi ni jukwaa la harakati, tunaunga mkono wanaharakati na jamii katika kuleta mawazo yao mbele.

Dalali **wa mamlaka na utawala** - sisi ni washawishi. Tunasema ukweli kwa nguvu, na tunashiriki madaraka kwa manufaa ya wote wanaopitia dhuluma na ukosefu wa usawa katika bara la Afrika.

Mtoa **huduma na mwezeshaji wa usaidizi wa kibinadamu** - tunatoa usaidizi wa dharura na kufanya kazi na jamii ili kupata ustahimilivu wa muda mrefu katika miktadha dhaifu na ya maafa barani Afrika.

## Mbinu zetu

**Ushirikiano** - tunashirikiana ndani ya Oxfam Barani Afrika, ikiwa ni pamoja na Ofisi za Nchi na Vikundi, pamoja na Washirika wa Afrika, Shirika pana la Oxfam, na washirika, wa ndani ya nchi na wa kikanda.

**Mashinani hadi kimataifa** - tunajihusisha katika viwango vingi na washirika wengi, kuunganisha sauti za mashinani hadi nafasi za kimataifa.

**Ushirikiano wa AU na REC** - tunadumisha uhusiano wa ndani/nje na kuunga mkono vitendo na kampeni za umma na washirika wetu.

**Kugawana uwezo** - tumejitolea kuchangia jamii ya kiraia ya Afrika yenye uthabiti, inayoshiriki kwa usawa ushauri wa kiufundi na usaidizi wa rasilimali pamoja na mshikamano wetu inapohitajika.

**Ushawishi na utetezi** - tunajihusisha na kampeni zinazoendeshwa na watu, kutumia uwezo wa vyombo vya habari na kusema ukweli kwa mamlaka na utawala.




Pascaline Namegabe, Afisa wa Afya ya Umma wa Oxfam, akionyesha eneo jipya la kunawia mikono la jamii katika makao ya wakimbizi waliokimbia makazi yao mjini Mwaka, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. *Picha ni kwa hisani ya: Arlette Bashizi/Oxfam*

# 6.0

# JINSI MABADILIKO YATATOKEA (NADHARIA YETU YA MABADILIKO)



HAKI NA USHIRIKI WA WATU
VIPAUMBELE
Kuondoa ukoloni
Mtazami wa ufeministi
Kuheshimu haki za kidijitali
UFADHILI
USHAWISHI
KUSHIRIKI KATIKA UJENZI WA UWEZO
Mtazamo wa kimfumo
Uwezo wa watu
Kufikiri kieneo na kutenda kimataifa
MATOKEO
Uwajibikaji katika utoaji wa huduma za kimsingi
Fungua nafasi ya kiraia
Mashirika thabiti ya utetezi wa haki za vijana na wanawake
Haki za fedha na ulipaji madeni
Mabadiliko katika haki za nishati
Biashara yenye usawa na jumuishi
Hatua za usaidizi wa kibinadamu wenye ufanisi
Mtazamo wa maeneo matatu msingi
Uwezo wa usaidizi wa kibinadamu uliobadilishwa
Mashirika thabiti ya kupigania haki za wanawake
Uhuru kutoka kwa vurugu za kijinsia
Ufikiaji wa huduma msingi
MATOKEO
Utawala jumuishi na wenye uwajibikaji
Ukuaji jumuishi na unaozingatia mabadiliko ya hewa
Utulivu wa kisiasa na kijamii
Maisha yenye heshima kwa wanawake na wasichana
ATHARI
AFRIKA YENYE USAWA
USHIRIKI, UWAJIBIKAJI, KUHESHIMU HAKI ZA WANAWAKE, WASICHANA NA VIJANA, HAKUNA TUTAKACHOJIFANYIA BILA SISI KUWEPO

# 7.0

# TUTAFANYA NINI (NGUZO ZETU TANO)

Kuwa na taswira ya Afrika iliyo na usawa tunayoshiriki kwa pamoja, ambapo kichocheo cha mabadiliko kimo katika jamii mbalimbali na zenye uthabiti za bara la Afrika. Katika kipindi cha miaka sita ijayo, OiA ina nafasi ya kuwa mshirika wa kutegemewa, ikishirikiana kwa karibu na washikadau wote wakuu ndani na nje ya Afrika ili kukabiliana na ukosefu wa haki na kukuza usawa.

Nguzo katika mkakati wa OiA zilichaguliwa kwa uangalifu kupitia mchakato wa kina ambao ulizingatia mahitaji ya wakazi wa Afrika huku ukizingatia kutumia uwezo, uzoefu na mafunzo kutoka kwa majukwaa ya awali ya kikanda ya Oxfam kama vile jukwaa la Pembe ya Afrika, Afrika Mashariki na Kati (HECA), Afrika Magharibi (WAF) na Mpango wa Pan-Afrika (PAP), pamoja na uzoefu na matarajio kutoka kwa Kitengo cha Kusini mwa Afrika (SAF) na Ofisi za Nchi. Mtazamo huu uliongozwa na uchunguzi wa hali halisi mashinani, pamoja na uchunguzi wa Mfumo wa Kimkakati wa Kimataifa wa Oxfam 2020–2030 na maarifa kutoka kwa Oxfam's Horizon 2 Roadmap. Kwa kuangalia mahitaji ya watu waliotengwa na maskini katika bara zima la Afrika, OiA ilitambua kuwa kushughulikia masuala ya kimfumo kama vile umaskini, ukosefu wa usawa na hali ya kuweza kuathirika ikiambatana na mazingira magumu kulihitaji nguzo zinazooana nguvu na utaalam ulioendelezwa kwa miaka mingi ya ushirikiano barani Afrika, lakini pia kuitikia mahitaji ya watu wa Afrika.

Mkakati huu utatekelezwa kupitia shughuli zinazotambua nguzo na malengo ya kimkakati. Katika kiwango cha shughuli, kila nguzo na nchi katika OiA inaweza kutumia viwezeshaji mbalimbali visivyo vya kawaida na kitamaduni kufikia malengo ya kimkakati yanayohusiana na ukosefu wa usawa na kupunguza umaskini. Hivi vinaweza kujumuisha kujihusisha na masuala ya umaskini wa mijini, uhamiaji, sekta ya kibinafsi na biashara za kijamii, na kutoa suluhisho za kiubunifu ambazo zinalingana na mahitaji maalum ya muktadha unaohusika. Viwezeshaji hivi vinaweza kuruhusu kila nguzo na nchi kutumia afua na mikakati yake na kuzifanya jumuishi zaidi na zenye matokeo yanayohitajika kule mashinani.



Seadiya Mohamed kutoka Tigray, Ethiopia, akichota maji karibu na nyumbani kwake baada ya Oxfam kusaidia katika ujenzi wa kituo cha kutolea maji. *Picha ni kwa hisani ya: Zerubabel Tore/Oxfam*




# 7.1 UCHUMI WENYE USAWA

**Kauli ya matarajio:** Afrika ambapo haki za kiuchumi za raia – wakiwemo wakulima wadogo, wafanyakazi na jamii za wachimbaji madini, kwa kuzingatia wanawake, wasichana na vijana - zinalindwa vikali na kupewa kipaumbele katika bara zima, na ambapo mashirika yanawajibishwa kwa utawala bora na ufaao.

Kuwaweka watu wa Afrika kama msingi wa chumi zinazowajibika na endelevu ni muhimu katika kupambana na ukosefu wa usawa.

## Maeneo ya kuzingatia

**Mifumo ya chakula na uhuru wa chakula, biashara na uongezaji thamani** – kufanya mifumo ya chakula na biashara na viwanda kufanya kazi kwa ajili ya watu wa Afrika.

OiA itashinikiza uhuru wa chakula, kutoa changamoto kwa mashirika ya kimataifa ambayo yamenasa mifumo ya chakula kwa nia ya kupata faida kubwa; pia tutahamisha mkazo kutoka kwa usalama wa chakula hadi uhuru wa chakula wa bara la Afrika.
Kwa kufanya kazi na mashirika na marafiki wa Afrika, tutafanya kampeni ya uwekezaji wa kutosha katika kilimo kulingana na Azimio la Malabo, ambapo Wakuu wa Nchi na Serikali za Afrika walijitolea kutenga angalau 10% ya bajeti zao za kitaifa kwa sekta ya kilimo. Pia tutatetea ushirikishaji na ujumuishaji bora wa wakulima wadogo katika mifumo ya kimakakati na yenye faida ya uongezaji thamani. Oxfam inanuia kutumia maendeleo yaliyofikiwa na maendeleo yajayo chini ya Mkataba wa Biashara Huria wa Bara la Afrika ili kukuza mifumo ya uongezaji thamani ya kilimo iliyojumuishi zaidi ili kuhakikisha kuwa wanawake na vijana wananufaika.

Tutatoa changamoto kwa mashirika ya pande nyingi na ya nchi mbili kuhusu jinsi yanavyounda uwekezaji wao ili kukuza uhuru wa chakula. Tutawaunga mkono watu wa Afrika kukabiliana na unyakuzi wa ardhi unaofanywa na serikali na makampuni ya kigeni, matajiri na wataajika wa kitaifa na sekta ya kibinafsi. Tutasaidia maendeleo na uimarishaji wa harakati za wakulima na kuongeza sauti zao. Tutatetea kwa ujasiri haki za wafanyakazi na mageuzi makubwa ya mazoea ya mashirika ili kuelekea manufaa ya haki, jumuishi na ya kimaendeleo.

**Haki ya Maliasili na mabadiliko ya nishati** – kukuza haki ya maliasili na kuhakikisha mapato ya haki na ugawaji wa faida.

Oxfam na washirika wake hawakufii mwoyo katika msimamo wao wa mapambano yao dhidi ya ukosefu wa usawa unaoendeshwa na viwanda vya uchimbaji madini na kudai mageuzi ya sera na mazoea ambayo yanakuza mgao wenye usawa wa mapato na manufaa ya maliasili. OiA itaunga mkono vitovu vya maarifa barani Afrika kufanya uchambuzi na utafiti wa sekta katika sekta nzima ya maliasili, ambao utatumika kupinga sera ya serikali na kukuza ushiriki wa watu wengi katika sekta hiyo. Tutakuza sauti za washirika na wadau wetu, tukitetea mabadiliko ya sera ambayo yanayapa kipaumbele mahitaji na haki za Jamii wenyeji kupata nishati, kushiriki katika maamuzi ya ardhi na rasilimali katika muktadha wa mabadiliko. Pia tutazingatia kuwawezesha wenyeji kutetea ardhi, maji na mazingira yao, na kutetea fidia ya haki na pia ridhaa ya awali yenye haki ya kupata na kupokea habari. OiA itatumia mikusanyiko ya kimkakati kama vile Mkutano Mbadala wa Indaba wa Madini wa Kila mwaka, Wiki ya Mafuta Barani Afrika, na majukwaa mengine ya kimataifa, barani na kitaifa ili kutetea mabadiliko makubwa kuelekea mazoea jumuishi na endelevu ya nishati. Tutaziwezesha Jamii Wenyeji na watu kutoka jamii asili kudai kupewa na kurejeshewa nafasi zao zinazostahili wakiwa katika mstari wa mbele katika michakato ya kufanya maamuzi.

## Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

- Kupitishwa na kutekelezwa kwa sera za kilimo na biashara za haki na zenye maendeleo zinazopendelea wakulima wadogo, wanawake, vijana, jamii wenyeji na makundi mengine yaliyo hatarini.
- Kuboresha mapato ya maliasili na ugavi wa faida unaolenga uwekezaji katika elimu, afya na ulinzi wa jamii.
- Sera zenye maendeleo zinazosimamia maliasili, sera zenyewe zikilenga suluhisho endelevu zinazoakisi mabadiliko ya nishati, mabadiliko ya hali ya hewa na haki za kijinsia, na kuyafanya mashirika na serikali kuwajibika.



Leticia anakausha maharagwe yake kwenye meza za kukaushia za kitamaduni zilizoko shambani mwake. Yeye ni mkulima mwanamke kutoka Ghana anayejitegemea ambaye anasimamia biashara yake mwenyew; biashara yake ya kuongeza thamani kwenye chokoleti peke yake. *Picha ni kwa hisani ya: Nana Kofi Acquah/Oxfam*



# 7.2 UTAWALA WENYE UWAJIBIKAJI NA JUMUISHI

**Kauli ya matarajio:** Afrika ambapo mifumo ya utawala ni jumuishi, yenye uwazi, na yenye kuwajibika kwa watu, inayolinda na kuendeleza haki za binadamu, maadili ya kidemokrasia na uendelevu wa mazingira katika bara zima.

Mifumo ya utawala yenye uwajibikaji na jumuishi ambayo inalinda haki za binadamu, maadili ya kidemokrasia na sayari yetu ni muhimu.

## Maeneo ya kuzingatia

**Nafasi za kiraia** – kukuza demokrasia inayowajibika, ya haki na shirikishi na jumuishi, inayotawaliwa na utawala wa kisheria, ambamo haki za msingi za binadamu zinalindwa na kukuzwa.

OiA pamoja na washirika wetu tutatetea vikali haki ya msingi ya uhuru wa kujieleza na kukutana. Tutapambana bila kuchoka dhidi ya ufisadi, kupinga majaribio yoyote ya kukandamiza nafasi za kiraia, na kupinga matumizi mabaya ya mamlaka ya kikatiba na kisiasa, ikiwa ni pamoja na kuondolewa na kupunguzwa kwa haki za wanawake na haki za wafanyakazi, ili kuhakikisha kwamba wale walio katika nafasi za mamlaka wanawajibika ifaavyo na kwa uthabiti. Kwa kuafikia haya, OiA itaunga mkono taasisi zote za Oxfam Barani Afrika, vyama vya wafanyakazi, mashirika na makundi ya utetezi ya wanawake, na washirika wa ndani, ikiwa ni pamoja na vyombo vya habari, kufanya kampeni ya uhuru wa kujieleza, kujumuishwa katika nafasi za maamuzi na juhudi za kuifanya serikali kuwajibika. Inapowezekana, OiA itatatetea kuhimiza serikali, AU na RECs kuhakikisha kwamba haki za kidemokrasia zinalindwa.

**Huduma za umma zenye uwajibikaji** – kufanya kampeni kwa ajili ya kupatikana, kwa huduma bora za umma, ikiwa ni pamoja na huduma ya afya, ulinzi wa kijamii na elimu kwa wote, ili kupunguza ukosefu wa usawa na kukuza maendeleo jumuishi na ya jamii.

OiA kwa ushirikiano na washirika wetu itatetea uwekezaji mkubwa zaidi katika huduma za kimsingi kwa kutilia mkazo kwenye uwekezaji katika huduma za afya, ulinzi wa jamii na elimu bora, kulingana na Mpango wa Utekelezaji wa Lagos. Tutakuza na kuunga mkono ujumuishaji wa haki za kidijitali na matumizi ya teknolojia katika mifumo ya elimu ya umma, na kuunga mkono mipango inayolenga kuhifadhi wasichana shuleni. Tutapinga ubinafsishaji wa huduma za kimsingi na mipango ya uchumi ambayo inapunguza uwekezaji katika huduma za kimsingi za umma na ulinzi wa kijamii. Kwa kufanya kazi pamoja na taasisi zote za Oxfam Barani Afrika na washirika wengine wakiwemo wasomi, vyama vya wafanyakazi na vyombo vya habari, tutatetea utekelezaji wa Azimio la Abuja kuhusu afya, ambalo linaweka lengo la 15% ya bajeti za kitaifa kuwekezwa katika huduma za afya na 20% ya bajeti ya kitaifa kuwekezwa katika elimu. Pia tutazisaidia jamii za kiraia katika maeneo ya ndani  na kujihusisha na michakato ya ufuatiliaji wa bajeti ili kuiwajibisha serikali

**Haki za kifedha na uendelevu wa deni** – kutoa wito kwa mifumo ya haki ya fedha inayounga mkono utozaji ushuru wenye uendelevu na ugavi wa mapato na manufaa yanayotokana na maliasili, na kupambana na mtiririko wa fedha haramu na hatua nyingine zinazochangia kuongezeka kwa ukosefu wa usawa.

Dhamira yetu ni kufichua mizigo ya madeni inayolemeza bara la Afrika, tukiangazia athari zake na kudai msimamo wa pamoja kuhusiana na msamaha wa deni. Tutapinga kikamilifu hali iliyopo katika masoko ya fedha ya Afrika, tukilenga wakopeshaji wakuu: serikali za G20, IFIs kama vile IMF na Benki ya Dunia, na sekta ya madeni ya kibiashara inayoendelea kukua. Oxfam itajiunga na kushirikiana na mitandao mikuu ya asasi za kiraia katika bara hili, kama vile Mtandao wa Haki ya Madeni wa Afrika, Mtandao wa Haki ya Ushuru Barani Afrika na Jukwaa la Afrika na Mtandao wa Madeni na Maendeleo, ili kupambana na mazoea makali ya upangaji wa kodi unaofanywa na makampuni makubwa na mashirika ya kimataifa. OiA, pamoja na taasisi zake, itaanzisha kampeni za kuangazia mizigo ya kitaifa ya kodi ya nchi moja moja na athari mbaya mizigo hii imekuwa nayo kwa matumizi ya umma. OiA itaunga mkono Ofisi za Nchi, Makundi na washirika wa maeneo husika ili kutetea sheria za kodi zilizo wazi na kanuni za uwajibikaji za kodi zinazopambana na ukwepaji wa ulipaji kodi na kukuza sera za haki za kifedha.

**Harakati za vijana na kijamii** – kukuza ugawaji wenye usawa wa uwezo wa mashirika ya vijana na harakati zingine za kijamii kwa kuuunga mkono mapambano yao ya kufanya kazi kwa uhuru na kujihusisha katika utawala wao wenyewe.

OiA itatoa rasilimali kwa ajili ya kujenga vuguvugu la vijana, vuguvugu la wafanyikazi na harakati zingine katika bara zima, hali itakayosaidia ubadilishanaji wa maarifa katika kanda na uimarishaji wa mitandao ya usaidizi. Tutatumia miunganisho yetu ya kimataifa kufungua nafasi kwa ajili ya harakati hizi ili kutangamana katika viwango vya kimataifa na bara. Kwa kufanya kazi pamoja na vyama vya wafanyakazi vya Afrika, Ofisi za Nchi, Vikundi na Washirika wa Kiafrika, tutazingatia kujenga vuguvugu la bara ambalo linajiimarisha na linajitegemea.

## Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

- Kupitishwa na utekelezaji endelevu wa mkataba mpya wa kimataifa wa kodi ulioongozwa na mataifa ya Afrika na mashirika ya kiraia.
- Kuongezeka kwa sera za kitaifa na kubuni sheria zinazohusu ukwepaji kodi na haki ya kulipa kodi katika bara la Afrika.
- Kupunguza mzigo wa madeni kwa nchi mbalimbali barani Afrika.
- Mashirika yote ya Oxfam Barani Afrika na washirika wa ndani ya Afrika kutayarishwa kufanya kampeni na kuwa wahusika wakuu katika masuala ya haki ya madeni katika

ngazi ya kitaifa. Raia zaidi wanajipanga katika harakati zinazofaa ili kukabiliana dhidi ya udikteta kutekwa kwa serikali na matajiri pamoja na wanaojiweza katika jamii na ubinafsishaji wa huduma muhimu - kudai haki, kupinga dhuluma na kutoa wito wa kuwepo kwa uwajibikaji.

- Kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika utawala, kunakodhihirika kupitia kuimarisha uhuru na uwezo wa asasi na taasisi mahususi za kidemokrasia, kiuchumi, kijamii na haki za binadamu na taasisi za kisheria.
- Mashirika thabiti zaidi ya vijana, vuguvugu la wafanyikazi na harakati zingine zinazoratibiwa na kujitegemea katika bara zima.
- Kuongezeka kwa uwekezaji katika huduma muhimu, haswa afya, ulinzi wa kijamii na elimu.
- Utoaji wa huduma za umma na serikali ulioimarishwa zaidi, haswa elimu na afya.
- Ujumuishaji ufaao wa mapendekezo yaliyotolewa na mashirika ya kiraia wakati wa Mapitio ya Kipindi cha Kimataifa cha Ukaguzi wa Kamishna ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Kibinadamu.



Huko Dotche Malam, Niger, mabinti wa Ramatou Adamou wanatabasamu huku wameketi nje kwenye kivuli na vitabu vyao vya shule. Licha ya kutoweza kwenda shule, Ramatou anawahimiza watoto wake kusoma, kupata maarifa na kufaulu maishani mwao. *Picha ni kwa hisani ya: Ibrahim Ousmane/Oxfam*



# 7.3 HAKI ZA ATHARI ZA MABADILIKO YA HALI YA HEWA

**Kauli ya matarajio:** Afrika ambayo inakabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa zinazoikabili na kuzishinda, ikitumia nguvu na sifa za watu wake mbalimbali na utajiri wa rasilimali zake ili kuunda mustakabali endelevu wa siku zijazo.

Haki ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa ni kitovu cha suluhu endelevu na thabiti kwa maisha na riziki.

## Maeneo ya kuzingatia

**Bidhaa za maarifa zinazomilikiwa na Afrika** – kuziba pengo la maarifa kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa.

OiA itashughulikia pengo la data katika usomi na tafiti za hali ya hewa kwa kukuza bidhaa za maarifa yanayomilikiwa katika maeneo husika ya bara la Afrika. Kwa kutambua wingi wa tafiti zilizoandikwa katika sehemu ya Kaskazini mwa Ulimwenguni, mkakati huu unalenga kufungua mitazamo ya Afrika, ikishawishi maamuzi ya hali ya hewa duniani. Juhudi hizi zinasisitiza kujitolea kupigania ujumuishaji na kuhakikisha kwamba changamoto za kipekee za muktadha wa Kiafrika ni muhimu katika mazungumzo ya mabadiliko ya hali ya hewa duniani.

**Mabadiliko ya sera** – kukuza hatua shirikishi za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa barani Afrika.

Kuna tofauti kubwa kati ya jamii, mashirika ya kiraia na watoa maamuzi. Oxfam na washirika watatetea mtazamo wa mabadiliko, huku wakianzisha jukwaa la mawasiliano ya moja kwa moja kati ya jamii Wenyeji na watunga sera. Njia hii inaruhusu ushiriki kikamilifu katika kubuni sera na mikakati ya ushawishi, inayopinga kanuni zilizopo. OiA itashirikiana na jamii, serikali, RECs na AU ili kuimarisha msingi imara unaotokana na ujumuishaji na upatanishi kwa ajili ya haki za mabadilko ya hali ya hewa zenye ufanisi.

**Kuwezesha ustahimilivu wa jamii za bara la Afrika na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko hali ya hewa** – kusaidia jamii za Afrika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

OiA itatoa kipaumbele katika kuwezesha jamii wenyeji kuendeleza mwitikio wao kwa mgogoro wa hali ya hewa, huku ikitambua changamoto zinazoingiliana za matukio yanayohusiana mabadiliko ya tabianchi na na hali ya hewa, mabadiliko ya soko la kilimo na maslahi ya serikali-shirika. Kupitia mipango mahususi ya upandaji miti na elimu kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa, tutaziwezesha jamii za mashinani, kutetea ustahimilivu na kukabiliana na hali hiyo. Tukiweka msisitizo thabiti kwa utaalamu wa maeneo husika na ndani ya jamii na uongozi wa wanawake, tutashirikiana na washirika mbalimbali kutekeleza ufumbuzi unaojumuisha kilimo kinachostahimili hali ya hewa, usimamizi endelevu wa maji na kupunguza hatari za maafa.

**Kukuza sauti za Afrika –** kutetea ufadhili wa kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, haki na usawa wa kimataifa.

OiA ikishirikiana na washirika wetu itatetea ongezeko la ufadhili wa kushughulikia mabadiliko ya hali ya hewa unaozingatia haki za binadamu mtazamo wa ufeministi barani Afrika, hili litashughulikia mzigo mkubwa wa tofauti zilipo barani Afrika. Tutaangazia hali

ya siasa za ufadhili wa mabadiliko ya hali ya hewa, inayotawaliwa na Nchi za Kaskazini mwa Ulimwenguni (Global North), na kuhimiza uwajibikaji wa matokeo yake. Tutakuza vuguvugu la kutetea mabadiliko ya hali ya hewa barani Afrika huku tukiunga mkono ushirikiano katika viwango mbalimbali, ikiwa ni pamoja na majukwaa ya kimataifa. Tutakuza uwepo wa Afrika na sauti ya Afrika kwenye majukwaa ya kimataifa, na kutetea sera za mabadiliko ya hali ya hewa zinazolingana na zinazokabiliana na tofauti za kijamii na za kiuchumi, huku tukiimarisha hoja zetu katika fikra za ufeministi na uondoaji wa mifumo ya ukoloni. Tukitenda kama mratibu, tutatetea ujumbe kutoka jamii na makundi yaliyotengwa ikiwa ni pamoja na wanawake, vijana na watu kutoka jamii asili na jamii wenyeji.

Kwa kuzingatia utetezi wa ufadhili wa mabadiliko ya hali ya hewa wa wanawake na wa kifeministi, ni muhimu kutambua majukumu ya kihistoria ya Mataifa ya Kaskazini mwa Ulimwengu katika muktadha wa mabadiliko ya hali ya hewa. Ukuaji wa viwanda na ukuaji wa uchumi wa nchi za Kaskazini ulijengwa kwa kiasi kikubwa kutokana na shughuli zinazotumia kaboni; shughuli ambazo zimechangia kwa kiasi kikubwa kwa mzozo wa mabadiliko ya hali ya hewa. Afrika, licha ya kuchangia kwa kiwango kidogo zaidi katika utoaji wa hewa chafu duniani, inakabiliwa na baadhi ya athari mbaya zaidi za mabadiliko ya hali ya hewa. Kanuni ya haki za mabadiliko ya hali ya hewa lazima ishughulikie ukosefu huu wa usawa wa kihistoria, ikihakikisha kwamba nchi ambazo zinawajibikia zaidi mabadiliko ya hali ya hewa pia zinabeba jukumu kubwa zaidi la kufadhili juhudi za kukabiliana na kupunguza makali ya mabadiliko haya Kusini mwa Ulimwengu. OiA itatetea uwajibikaji kutoka Nchi za Kaskazini mwa Ulimwengu katika kutimiza ahadi zake za ufadhili wa mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na kushughulikia jukumu lake la kihistoria katika kuendeleza dhuluma za kimazingira.

## Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

- Mijadala ya sera na maamuzi ya watunga sera kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa inayolenga mabadiliko ya haki, uwepo wa usawa na inayozingatia nafasi ya wanawake.
- Ufadhili zaidi kushughulikia mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi unaolenga watu, unaopatikana na kufikika na unaotabirika.
- Utafiti mpya na data kuhusu mwitikio wa Afrika na athari za mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi kwa Afrika ambao utatumika kama kichocheo cha kuongeza ufikiaji wenye usawa kwa nishati mbadala na safi inayozalishwa kwa uwajibikaji; na uondoaji wa haraka, wenye haki na unaofadhiliwa mafuta ya visukuku.
- Kuibuka na kuimarishwa kwa harakati zinazoingiliana zinazotetea haki za mabadiliko ya hali ya hewa katika bara la Afrika. Kuimarisha uzalishaji na mapato ya kilimo endelevu, kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi.



Kundi la wafugaji na mifugo wao wanawasili katika jamii ya Sincaro, Somalia, ambapo Oxfam imejenga mfumo wa kusambaza maji kwa watu na wanyama. Sincaro ni eneo la kimkakati kwenye njia za transhumance. *Picha ni kwa hisani ya : Pablo Tosco / Oxfam Intermón*



# 7.4 HAKI ZA KIJINSIA

**Kauli ya matarajio:** Bara ambalo watu wanaishi bila dhuluma za kijinsia, na wanawake na wasichana wanarejeshewa na kupata haki zao na kuishi kwa utu.

Maisha yenye heshima yasiyo na ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia ni haki ya kimsingi ya binadamu ambayo ni msingi wa maendeleo na usawa wa binadamu. Utambuzi na ulinzi wa haki zenye usawa za wanawake lazima uzingatiwe kuwa msingi wa kufikia malengo mengine yote ya maendeleo ya binadamu na haki za kijamii. Haki za wanawake sio tu suala la haki bali ni sharti la lazima ili kuwepo na maendeleo endelevu katika nyanja zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kwa hivyo, haki zenye usawa wanawake ndio msingi ambao jamii jumuishi, thabiti na zenye haki zimepata msingi wake, na ndio lengo kuu la mkakati huu.

## Maeneo ya kuzingatia

**Unyanyasaji wa kijinsia wa kimuundo na wa kimfumo** – kuhakikisha jamii barani Afrika ziko salama na hazina unyanyasaji wa mfumo wa ubabedume, wa kimuundo, ubaguzi, upendeleo, sheria zenye madhara na harakati za kupinga haki zinazolenga wanawake na wasichana.

OiA itatetea uundaji na utekelezaji wa sera na utendaji zinazosisitiza mabadiliko ya kijinsia katika ngazi ya kitaifa na kikanda, na hii ni pamoja na kuunga mkono mashirika ya Oxfam Barani Afrika ili kuendeleza utetezi wa sera katika ngazi za kitaifa. Tutashirikisha sekta ya kibinafsi na IFIs katika kuunda mikakati na mipango inayolenga masuala ya kijinsia.
OiA pia itahakikisha kwamba mitazamo, kanuni na mifumo ya imani yenye madhara ambayo huongeza unyanyasaji na kuwaweka wanawake wakisalia kuwa wasio na usalama, maskini na waliotengwa inapingwa na kubadilishwa. Mikakati itajumuisha kuwashirikisha wanaume na wavulana kubadilisha kanuni za mfumo wa ubabedume na kukabiliana na hadithi kutoka kwa wanaharakati wanaotumia mifumo ya kidijitali kupinga haki zinazoendeleza unyanyasaji dhidi ya wanawake.

Tukishirikiana na washirika wetu tutachangia, tutaunda na kushawishi maendeleo na lugha ya sera za AU. Tutashirikisha taratibu za haki za binadamu za Umoja wa Mataifa na AU na utaratibu maalum katika kufuatilia utekelezaji wa mifumo ya kisheria ya nchi wanachama kama vile Itifaki ya Maputo. Katika programu zetu, tutahakikisha kwamba waendelezaji wa unyanyasaji wa kijinsia wanawajibikia vitendo vyao, na kuhakikisha kwamba waathiriwa na waathirika wanapata huduma na usaidizi wa hali ya juu.

**Uongozi wa wanawake wenye mabadiliko** – kukuza utetetezi wa haki za wanawake/ufeministi uliojumuishi zaidi, wenye usalama na wenye uhai na unaombatana na rasilimali za kutosha, ukiambatana na nafasi za utetezi wa kiraia kwa ajili ya shughuli za kuwatetea wanawake zinazohakikisha ushiriki wa watu wote.

OiA itawezesha, itauunga mkono na kuhimiza haki sawa za wanawake na mashirika na harakati za kutetea haki za wanawake ili kuchangia, kuunda na kushawishi sera za mabadiliko ya kijinsia katika ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Tutawaunga mkono, tutajifunza kutoka kwao na kuinua mashirika yao na sauti zao katika kazi zote tunazofanya mtandaoni na nje ya mtandao.

Pia tutachangia, tutaunda na kuathiri hadithi za sera kwa ushirikiano na washirika na harakati mbalimbali katika majukwaa ya bara na ya kimataifa. Tutashiriki katika utafiti unaohusiana na masuala ya wanawake na mafunzo kupitia utayarishaji wa mihtasari ya sera na mihtasari ya uchanganuzi wa kitaalamu, na kuunga mkono ujumuishaji wa

muktadha wa Afrika katika utafiti wa Shirika la Oxfam. OiA pia itasaidia mashirika ya watetezi wa haki za wanawake kutetea nafasi ya kiraia kwa ajili yao kufanya kazi na kulindwa dhidi ya upinzani mkali dhidi ya haki za binadamu.

**Haki ya kiuchumi ya kijinsia na utunzaji** – Haki ya kiuchumi ya kijinsia na utunzaji - kuendeleza miundo mbadala ya kiuchumi ya kifeministi ambayo inazingatia huduma, usawa na ustawi kwa wote kama njia mbadala ya mifumo ya sasa ya ubabedume, uliberali mamboleo na unyanyasaji. OiA itakuza hadithi za wafeministi na hadithi mbadala kuhusu masuala ya mada, yakiwa ni pamoja na utunzaji, haki za kifedha na haki za mabadiliko ya hali ya hewa, kupitia midahalo na majopo ya wataalamu.

Tutaendeleza ushirikiano wetu na Benki ya Dunia kuhusu sera ya ulinzi na haki za kijinsia, pamoja na majukwaa mengine ya ndani ya maeneo ambapo mazungumzo yanaendelea. Tutatumia fursa iliyotolewa na Benki ya Afrika ya Maendeleo ya kuendeleza utetezi wa masuala ibuka katika kazi ya Oxfam kuhusu ulinzi na tutakuza na kuendeleza the Care Barometer.

**Haki za Afya ya Uzazi (SRHR)** – kuhakikisha kwamba haki za afya ya uzazi zinatolewa, zinaweza kufikiwa na zinaheshimiwa katika bara zima.

Kwa kufanya kazi na mashirika ya watetezi wa haki za wanawake katika bara zima, OiA itachangia katika kubadilisha kanuni za kijamii kwenye SRHR zinazolenga kuongeza uhuru wa mwili wa wanawake na wasichana, mashirika na ustawi wao. Pia tutajitahidi kukuza mtazamo chanya na wenye heshima kwa mahusiano ya kijinsia, pamoja na kuwekeza vya kutosha katika huduma za afya ya ngono na uzazi.

## Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

- Kuidhinishwa, kuanzishwa na kutekelezwa kwa Itifaki ya Maputo kukichukua hatua kuu katika nchi nyingi za Afrika. Kutambua, kupunguza na kugawa upya ulinzi wa nyumbani usiolipwa na kazi za nyumbani zinazokuzwa kupitia kampeni za bara na kitaifa. Oxfam itajiunga na miungano ya kibara yenye rasilimali nyingi ambayo inafanya kampeni kikamilifu kwa ajili ya kuvunjwa kwa kanuni na desturi za mfumo wa ubabedume.

- Michango muhimu ya OiA na washirika wake katika mapitio ya miaka 30 ya Jukwaa la Utekelezaji la Beijing na michakato mingine muhimu ya sera ya jinsia. Utumiaji madhubuti wa lenzi ya kijinsia kwa michakato na sera zote za ndani.





# 7.5 HATUA ZA USAIDIZI WA KIBINADAMU

**Kauli ya matarajio:** Hatua za usaidizi wa kibinadamu zinazolenga kushughulikia mizizi na visababishi msingi vya usaidizi wa kibinadamu na kuwawezesha watu walioathirika kuchukua uongozi ili kufikia matokeo ya kudumu na kujenga upya maisha yao.

Mtazamo wa uhusiano unaoleta pamoja vijenzi vitatu; shughuli za usaidizi wa kibinadamu, maendeleo na ujenzi wa amani katika programu zote na ushawishi ni msingi wa kufikia suluhu endelevu katika hali za shida.

## Maeneo ya kuzingatia

**Mwitikio wa kibinadamu madhubuti, wa kiubunifu na wenye kuzingatia kanuni za kibinadamu** – kuhakikisha mwitikio uliojitosheleza na unaokuja kwa wakati katika nyakati za majanga. Msingi wa mwitikio wa Oxfam bado unasalia kuwa usalama wa dharura ya chakula (EFS), maji, mazingira safi (WASH), na ulinzi. Oxfam itawasaidia washirika wake kukusanya rasilimali kwa ajili ya kuchukua hatua huku ikipinga maamuzi ambayo yanaweza kupunguza upatikanaji wa ufadhili, ikipanua vyanzo mbalimbali vya ufadhili, ikitetea ufadhili wa miaka mingi, na kuhakikisha kuwa wahusika wa ndani wanafadhiliwa vya kutosha.

Pia tutahimiza na kuboresha ushiriki wa maarifa kote katika kanda na nchi, tukikuza uvumbuzi, kuwekeza katika kujifunza kutoka kwa wenzetu, na kufuatilia mbinu zetu kwa kutumia kanuni za utetezi wa haki za wanawake. Ubunifu utakuwa muhimu, na tutachunguza matumizi ya teknolojia ili kusaidia kutoa mwitikio wa kibinadamu wenye ufanisi. Washirika muhimu katika bara la Afrika (mbali na INGO muhimu) wakijumuisha mtandao wa Africa START network na Mtandao mpya ulioanizishwa wa Mashirika ya Kibinadamu ya Afrika (AHON), ambayo Oxfam tayari ni sehemu ya uongozi wake, pamoja na mashirika ya Umoja wa Mataifa, RECs na mashirika mengine ya kikanda.

**Utayari** – kuhakikisha mipango madhubuti na iliyo na rasilimali za kutosha katika programu zote.

OiA itahakikisha kwamba Ofisi za Nchi/Ofisi za Vitengo na washirika wake, pamoja na Washirika wa Afrika, wana rasilimali wanazohitaji ili kushiriki katika kazi ya kujitayarisha kama vile uchunguzi wa hali, uchambuzi wa hatari na upangaji wa dharura. Tutashirikiana na jamii na washikadau wenyeji katika kutathmini hatari zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa ili kujumuishwa katika mipango ya utayari, na kushawishi wafadhili kujumuisha utayari katika ufadhili wao.

OiA itafanya ukaguzi wa mifumo ya kufanya maamuzi, itifaki, taratibu na uwajibikaji, kwa kutumia lenzi ya kuondoa ukoloni na kuwekeza katika maeneo ambayo yanahitaji uboreshaji. Pia tutalenga kuongeza uwekezaji katika taratibu zinazotarajiwa za utekelezaji, tukiziunganisha na taratibu za ulinzi wa jamii.

**Kuunganisha mwitikio wa kibinadamu na athari za muda mrefu** – kuhakikisha kwamba manufaa ya mwitikio wa kibinadamu yanadumishwa na maisha ya watu yanajengwa upya.

OiA itatoa kipaumbele kwa kufanya uchanganuzi thabiti zaidi wa muktadha; uchanganuzi utajumuisha mitazamo kuhusu mienendo ya uongozi na utawala, usawa wa kijinsia, lengo kuu likiwa ni kuzingatia mahitaji ya jamii. Kwa kushirikiana na wadau wa ndani ya maeneo kama vile Mashirika Yasiyo ya Serikali (NGOs), mashirika ya kitaaluma na kielimu na sekta ya kibinafsi, tutalenga kuimarisha ubora wa uchambuzi wetu ili kuhakikisha ufanisi wa kudumu wa mikakati na afua zetu. Kwa kutumia mtazamo wa kimfumo, tutalinganisha juhudi zetu za kibinadamu na hatua za ziada zinazoshughulikia vyanzo na sababu za

msingi za migogoro. Msisitizo wetu utakuwa katika kuimarisha taasisi, ikiwa ni pamoja na za taasisi za ndani ya maeneo yanayopokea usaidizi, pamoja na mifumo na uwezo ufaao kwa ajili ya suluhisho zinazotokana na uvumbuzi endelevu.

**Kubadilisha mifumo ya utawala na uongozi** – kuhakikisha mabadiliko ya mifumo na michakato ya usaidizi wa kibinadamu, ya ndani na nje, ili kufikia hatua za kibinadamu zenye haki, usawa na za kuleta athari kwa maisha ya binadamu.

OiA imejitolea kuchukua jukumu kuu katika kubadilisha mifumo ya utoaji wa misaada ya kibinadamu ili kuifanya iwe na ufanisi zaidi. Pia imejitolea kuunda nafasi za kuchunguza na kutoa changamoto kwa fikra na utamaduni wetu wa shirika wa usaidizi wa kibinadamu, na kuendeleza maono na uelewa wa pamoja wa thamani inayoongezwa na Oxfam katika kuondoa ukoloni katika kazi ya usaidizi wa kibinadamu, huku tukihakikisha kwamba tusilete madhara. Katika shirika la Oxfam, tutazingatia kubadilisha mifumo ya ndani, haswa mifumo yetu ya biashara, ili iwe yenye kasi zaidi hasa katika masuala ya kuunga mkono kazi ya usaidizi wa kibinadamu. Tutatetea suluhu zinazoongozwa na wenyeji, na kutoa changamoto kwa nafasi inayopungua ya usaidizi wa kibinadamu na ya kiraia, na kuangazia upatikanaji wa usalama wa misaada wenye kutotegemea msimamo wa kidini na hali ya kuwepo kwa viwango na kanuni zisizotumika kwa usawa. Nje ya shirika, tutapinga mienendo ya uongozi na utawala ya ukandamizaji na isiyo ya haki, tutakuza mtazamo wa wanawake na usawa wa kijinsia kama suala la msingi. Tutatetea na kuwekeza katika uongozi wa mitaa, na kuheshimu maarifa na uongozi wa wenyeji kwa ajili ya thamani uongozi huo unaleta.

## Je, mafanikio yatakuwaje ifikapo 2030?

- Mwitikio wa Oxfam kwa masuala ya kibinadamu unachangia katika kupatikana kwa haki sawa za wanawake.
- Oxfam inaitikia kwa haraka na kwa kiwango kikubwa ikilinganishwa na kuzorota kwa viashiria vya kibinadamu kulingana na haki za binadamu za kimataifa pamoja na sheria za wakimbizi na za kibinadamu.
- Oxfam inaonyesha mtazamo wa usifanye madhara na mtazamo wa maandalizi salama ya mapema katika afua na mikakati yake yote.
- Juhudi za kibinadamu, za kimaendeleo na za ujenzi wa amani za Oxfam zinalingana na uwezeshaji wa wanawake, uongozi na mashirika.
- Afua zote za Oxfam za moja kwa moja zinasaidia na kuunga mkono mifumo ya kitaifa na ya maeneo husika katika hatua za kibinadamu, bali sio kubadilisha nafasi ya uwezo ulipo.
- Ufadhili ulioongezeka, unaotegemewa na unaopatikana kwa urahisi unaoweza kutolewa

kwa wakati unaofaa ili kuokoa maisha.

- Ufadhili baina ya nchi mbili na wa kimataifa unasaidia juhudi zifaazo jamii husika na mitazamo ya kufanya kazi kwa ushirikiano na mashirika mengine imeongezeka kwa kiasi kikubwa.
- Oxfam inaongoza katika kujenga uongozi wa kibinadamu wa eneo husika kupitia utekelezaji unaoongozwa na washirika wa jamii na eneo husika, hali itakayosaidia mitandao ya kibinadamu ya Afrika na mashirika kama vile AHON, na kufanya fedha na pesa na ufadhili wa haraka wa kukabiliana na dharura upatikane kwa mashirika ya kiraia, na hivyo kujiweka kama sauti kuu katika kuunda suluhisho zinazofaa jamii za bara la Afrika.




Mkimbizi Asia* akinawa mkono katika kituo cha WASH kilichofadhiliwa na Oxfam kwenye kambi yao katika kituo cha usafiri huko Renk, Sudan Kusini. *Picha ni kwa hisani: Peter Caton/Oxfam* **Jina limebadilishwa kwa kuzingatia miongozo ya maudhui ya maadili ya Oxfam*

# 7.6 MTAZAMO WA MASUALA YANAYOINGILIANA

Tunakubaliana na Mfumo wa Kimkakati wa Oxfam wa Kimataifa kwamba jinsi tunavyofanya kazi ni muhimu kama vile tunachokifanyia kazi. Kubadilisha jinsi tunavyofanya kile tunachokifanya kutatufanya kuwa na umuhimu zaidi na wenye ufanisi zaidi katika bara la Afrika, kulingana na matarajio ya washirika na marafiki wa Afrika. Lenzi zifuatazo zinaonyesha kazi zetu zote, na tutazitumia kote ili kuhakikisha kuwa zinaarifu kila kitu tunachofanya.

## Kuondoa ukoloni

Mifumo ya sasa ya kiuchumi, kisiasa, kitamaduni na maarifa ni urithi wa mamlaka ya kikoloni katika bara zima la Afrika. Mifumo ya kimataifa, ambayo ipo kwa kiasi kikubwa barani Afrika, inaimarisha mahusiano ya mamlaka ambayo ni ya mfumo wa ubabedume, ubaguzi wa rangi na unyonyaji, hali inayoimarisha na kudumisha ukosefu wa usawa wa kimfumo. Utawala na uongozi umelimbikizwa katika mataifa ya Kaskazini ya Ulimwenguni na hudumishwa kupitia uhusiano wa kibiashara, kisiasa na misaada.

**Matumizi:** Oxfam inafanya kazi kwa utaratibu ili kuondoa ukoloni katika kazi yake kama sehemu ya mchakato mkubwa wa kuondoa ukoloni ambao ni muhimu ili kukabiliana na ukosefu wa usawa wa kimataifa na wa ndani ya nchi za Afrika. Sambamba na juhudi hizi, OiA itazingatia kusawazisha ubia na kuendeleza kazi muhimu ya kurekebisha mbinu za ufadhili. Tutashughulikia matumizi ya lugha, desturi za kuajiri na uwazi kuhusu taarifa za fedha. Zaidi ya hayo, tutaendelea kutetea ndani ya Oxfam kupata utawala sawa  katika kufanya maamuzi, na kuhama kutoka kwa kusisitiza na kuthamini mazoea ya Nchi za Kaskazini mwa Ulimwengu. Hii ni pamoja na kuanza kutumia aina mpya za mbinu za Asilia, kama vile usimulizi wa hadithi na simulizi za kitamaduni, na bidhaa zingine za maarifa ili kuchukua jukumu kuu. Oxfam kama shirika, na hasa katika jukumu lake kama INGO, linajitolea kutembea kwa uangalifu ili kuepuka kuendeleza miundo ya mamlaka iliyopo, na kutumia lenzi ya kuondoa ukoloni katika mwingiliano hali na mbinu zake nyingine ili kuhakikisha kwamba miundo ya uongozi inaimarishwe. Oxfam italenga kuwa sauti thabiti ya bara kuhusu mabadiliko ya utawala katika masuala ya misaada ya kibinadamu na ushirikiano wa kimaendeleo. Hasa kama sauti ya Afrika, Oxfam itashinikiza kuchukua hatua na mabadiliko ya kweli katika ya harakati za kuondoa ukoloni, mbali na mjadala tu na kutochukua hatua.

## Mtazamo wa ufeministi

Miundo ya mfumo wa ubabedume inakandamiza wanawake na wasichana katika nafasi mbalimbali za kijamii. Miundo hii, pamoja na mienendo isiyo sawa ya utawala na uongozi, husababisha wanawake na wasichana, idadi inayojumuisha watu wengi, kuishi katika umaskini. Katika mfumo wa ubabedume, wanaume wanashikilia mamlaka na wanafafanua majukumu ya kijinsia, mara nyingi hali hii husababisha kutii na kunyenyekea kwa wanawake.

**Matumizi:** Mbinu ya ufeministi ya Oxfam inakabiliana na ukosefu huu wa usawa kwa kutumia kanuni zake msingi za ufeministi. Barani Afrika, Oxfam itazingatia hali ngumu ya mienendo ya utawala na uongozi na kuunganisha hili katika upangaji wake. Kutokana na kukithiri kwa dhuluma za kiume, kuna haja ya kuwashirikisha wavulana na wanaume ili kutoa changamoto na kubadilisha maadili haya yenye madhara ambayo yanaendeleza ukosefu wa usawa wa kijinsia na ukatili. Kwa kifupi zaidi, lengo letu ni kuhakikisha usawa wa kisheria kati ya wanawake na wanaume. Katika kazi yetu, tumejitolea kuchunguza na kushughulikia aina zote za ubaguzi, dhuluma na ukiukaji wa haki unaowapata wanawake na wasichana. Tutajitahidi kutekeleza mtazamo wa ufeministi katika desturi zetu za kuajiri na kuhakikisha kuwa taratibu zetu za programu zinazingatia masuala ya kijinsia.

## Kuheshimu haki za kidijitali

Mazingira ya kidijitali barani Afrika yanaongezeka. Afrika inaongoza duniani kwa kuwa na watu wanaopata intaneti kupitia simu zao za mkononi. Hii ina uwezo mkubwa kwa Afrika kuziba ukosefu wa usawa na kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu. Hata hivyo, ufikiaji usio sawa wa kidijitali na matumizi mabaya ya teknolojia ya kidijitali huzidisha ukosefu wa usawa na ubaguzi.

**Matumizi:** Ahadi ya Oxfam ya kutetea haki za kidijitali barani Afrika imo ndani ya muktadha wa teknolojia ya habari na mawasiliano kwa ajili ya maendeleo (ICT4D), kwa sababu tunaamini kuwa hii inakuza uanaharakati miongoni mwa raia na kuwezesha na kulinda uwasilishaji wa ustawi wa jamii na misaada ya kibinadamu. Lengo letu ni kuhakikisha ufikiaji wenye usawa na miundombinu ya kidijitali yenye gharama ya nafuu, zana na nafasi za mtandaoni, na kuchukua jukumu muhimu katika kupanua na kutumia nafasi za kidijitali, huku tukifanya kazi na wanaharakati wa kidijitali wachanga na wa kike.

## Umoja wa watu

Miundo ya kiuchumi na kisiasa inaweza kufanya kazi ili kudhibiti mamlaka na kuzima sauti za watu wa kawaida. Ndivyo ilivyo kuhusiana na usaidizi wa maendeleo na misaada ya kibinadamu, na uwezo wa watendaji wa Nchi za Kaskazini mwa Ulimwengu zinazozidi sauti na mahitaji ya wale ambao wameathiriwa zaidi na ukosefu wa usawa na umaskini. Ingawa kuna mila thabiti za mamlaka ya watu na mikabala shirikishi katika bara la Afrika, hizi mara nyingi hufunikwa na kupuuzwa na mifumo inayotawala kisiasa na kiuchumi.

**Maombi:** Katika Afrika, jukumu la Oxfam la kufanya kazi na kukuza sauti za jamii zilizotengwa litakuwa kipengele muhimu cha kubadilisha mahusiano ya mamlaka. Pamoja na washirika wetu, tutatoa changamoto kwa watu mashuhuri katika siasa na uchumi ambao wana mamlaka yanayoonekana na yasiyoonekana katika nchi nyingi za bara hili, na Oxfam itatumia uwezo na fursa yake kufungua nafasi za kutangamana na watu mashuhuri na matajiri hawa. Kuunga mkono mipango ya ndani na kukuza mitandao ya mashinani ni muhimu ili kuziwezesha jamii.

Tunaahidi kuunga mkono na kusimama pamoja na wale wanaopigana dhidi ya kutengwa, unyonyaji, umaskini na migogoro. Tutatoa usaidizi wa moja kwa moja inapohitajika na kushirikiana nao ili kuunda maabadiliko chanya, ikiwa ni pamoja na kutetea haki zao. Zaidi ya hayo, tutawekeza katika uongozi, uhuru na uwezeshaji wa vijana.

## Kufikiri kieneo na kutenda kimataifa

Wamiliki wa miundo ya utawala na uongozi wapo katika ngazi za kimataifa, kikanda na za mitaa. Miundo hii ya utawala imeunganishwa na kuimarishwa kwa pamoja. Kukabiliana na miundo hii ya utawala ambayo ni changamano, zenye ngazi mbalimbali na zinazoathiri sekta nyingi inahitaji ujenzi wa kitaratibu wa miungano ambayo inatoa nguvu sawa kutoka ngazi zao husika - kimataifa, kikanda na mitaa.

**Matumizi:** OiA itakuwa kiungo imara zaidi cha kukuza sauti za watendaji wa ndani na maeneo husika katika kampeni na utetezi wa bara na kimataifa, pamoja na kuunganisha ujuzi wao wa ndani na mijadala ya kimataifa. Hili ni muhimu zaidi wakati wa kushughulikia changamoto kubwa za kimataifa, kama vile usawa wa kijinsia, madeni na mabadiliko ya hali ya hewa.

## Mbinu ya kimfumo

Utawala unaoendeleza umaskini na ukosefu wa haki unashikiliwa katika mifumo – mifumo hii ni ya kikoloni, ya ubabedume, matajiri na watu maarufu katika jamii na wengineo - na Afrika haiwezi kukwepa hili. Ili

kuleta mabadiliko yenye maana, endelevu na kuhamisha utawala kutoka kwa wamiliki waliopo, mifumo yenyewe inahitaji kubadilishwa.

**Matumizi:** Matatizo ya kimfumo yanahitaji suluhu za kimfumo, na Oxfam itafuata usawa wa kimfumo. Hii ni kweli kwa Afrika, ambapo mifumo imezaliwa na kukita mizizi katika jamii na kupata sura mbalimbali. Katika hali ambapo mbinu za pande nyingi zinahitajika ili kukabiliana na mifumo ya ukosefu wa usawa, ukosefu wa haki na ubaguzi, OiA imejitolea kuchanganua mifumo na mabadiliko ambayo yanahitaji ushiriki wa muda mrefu na thabiti. Nguvu za ujifunzaji wa pamoja na maarifa ni kichocheo kikuu cha kubadilisha mifumo. Barani Afrika, Oxfam itaunda majukwaa ya kuwezesha kujifunza kwa pamoja, ujifunzaji wa mengi zaidi ya mipaka ya kijiografia na vizuizi vya lugha.

## Utekelezaji wa mkakati

Mkakati wa OiA utatekelezwa kupitia nyaraka za kina za nguzo za programu, mikakati mahususi ya nchi na ufafanuzi wa kazi muhimu za usaidizi. Kila nguzo itakuwa na hati maalum za programu zinazoelezea malengo, mbinu na matokeo yanayotarajiwa. Mikakati ya nchi itawekea nguzo hizi muktadha, ikihakikisha upatanishi na hali halisi ya ndani ya nchi na mahitaji. Zaidi ya hayo, vipengele muhimu vya usaidizi kama vile Rasilimali Watu, Uendeshaji, shughuli na Ufuatiliaji na Tathmini vitafafanua mbinu zinazofaa ili kutoa miundombinu muhimu kwa ajili ya utoaji wa programu kwa ufanisi. Mbinu ya ushirikiano pia itaandaliwa ili kuhakikisha kuwa ushirikiano na mashirika ya ndani, mashirika ya serikali na washikadau wengine unawiana na malengo ya mkakati.

Mbali na kutekeleza mkakati huu kupitia nyaraka za nguzo za programu, mikakati ya nchi na vipengele vya usaidizi, OiA itashirikiana kwa karibu na Washirika wa Afrika na Kitengo cha Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini (MENA) kuhusu ushawishi wa kikanda wa Pan-Afrika. Ushirikiano huu utazingatia vipaumbele vya pamoja, huku ukihakikisha kuwa juhudi za utetezi wa kikanda ni zenye mshikamano imara na zenye athari na matokeo thabiti. OiA itashirikiana zaidi na Washirika wa Afrika ili kutumia utaalamu wao na mitandao ili kuongeza juhudi za kushughulikia ukosefu wa usawa na umaskini. Ushirikiano huu utaimarisha mafunzo ya kikanda, kuimarisha kazi ya utetezi ya pamoja ya Oxfam, na kuhakikisha kuwa mkakati unaonyesha mtazamo wa pamoja wa kuathiri mabadiliko ya sera na ya kimuundo katika ngazi za kikanda na za bara.




Wafanyakazi wa kujitolea wakiwa wamebeba picha zilizochapishwa mbele ya magari yaliyosimamishwa karibu na taa kwenye msafara wa matembezi ya mabadiliko ya hali ya hewa tarehe 13 Oktoba 2022 katika makutano ya Allen, Ikeja, Jimbo la Lagos, Nigeria. *Picha kwa hisani ya: Taiwo Aina / Oxfam*

# 8.0

# ATHARI ZA MKAKATI HUU KWA OXFAM BARANI AFRIKA

Kuidhinishwa kwa mkakati huu kutakuwa na athari kwa uendeshaji wa OiA na mahusiano yake ya ndani ya shirika; na kutekeleza matarajio ya mkakati kutahitaji marekebisho na mabadiliko katika shirika. Wakati huo huo, ni muhimu kutambua kwamba sehemu nyingi za mkakati huu zimetokana na kazi zilizopo ambayo zinaweza kuhitaji kukuzwa, kuwezeshwa na kuimarishwa.

## Kurekebisha njia zetu za kufanya kazi

Uwezo wa OiA kutekeleza mkakati huu upo katika utofauti wake. Kwa vyombo tofauti vinavyounda OiA, inahusisha zaidi ya kupanga tu mkakati: inamaanisha kutimiza vipengele maalum vya mkakati, kujenga kwenye uwezo wao wenyewe ili kupata athari za juu zaidi.

Matarajio yetu ni Oxfam Barani Afrika ambayo:

- Ina ushawishi, kwa kuunganisha miundo ya kitaifa, kikanda na kibara kwenye sehemu tofauti za Oxfam International na Shirika zima.
- Inaongeza ushiriki kutoka Afrika ili kufahamisha michakato ya Oxfam International.
- Inachangia kikamilifu katika kampeni za kimataifa za Oxfam.
- Inaanzisha uhusiano wenye athari na manufaa kwa Washirika.
- Imedhamiriwa kuunda uhusiano mpya na washirika wa Afrika na kuchukua nafasi yake kama INGO.

Ili kufikia azma hii, OiA itabidi iwe na maksudi katika kubainisha nafasi zenye manufaa miongoni mwa taasisi zake mbalimbali - kama vile nafasi ya Oxfam Afrika Kusini na BRICS na G20, na nafasi ya Kitengo cha Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) - na kuzitumia kwa faida kubwa za kuboresha programu. Kwa uwazi zaidi wa kiutendaji, matriksi ya uwajibikaji itachorwa na kukaguliwa mara kwa mara kama sehemu ya uendeshaji wa mpango wa kila mwaka au mikakati/mipango mahususi ya kampeni.

## Mifumo na taratibu

Oxfam imeendelea kubadilika na kurekebisha mtazamo wake wa upangaji programu, lakini mifumo ya biashara imebaki nyuma. Mpango wa sasa wa Mfumo wa Kubadilisha Biashara (TBS) ni muhimu kwa uendeshaji bora wa OiA na sehemu nyingine za Shirika zima. OiA itasaidia katika kuleta mabadiliko ya mifumo ya biashara kote kwenye Oxfam kwa ajili ya ubora wa kiutendaji na kuondoa ukoloni kwenye mifumo na ushirikiano wa kifeministi, hivyo kuwezesha athari kubwa kutoka nje. Tutashiriki uzoefu na mafunzo yetu katika kufanya kazi na mifumo ya sasa ya biashara, kuchambua athari za mifumo ya sasa dhidi ya OiA mpya iliyowekwa, na kushiriki mapendekezo na Shirika la Oxfam.

## Watu wa Oxfam

Oxfam imejitolea kuwajali watu wake na kudumisha utamaduni wa kupinga ubaguzi wa rangi, uondoaji ukoloni, utamaduni wa ufeministi ili kuheshimu na kuwawezesha watu, kukuza uongozi wa wanawake na kuongeza athari za pamoja. OiA itakuwa makini katika kufuatilia dhamira ya shirika ya kurekebisha njia zake za kufanya kazi kwa kuhamisha mamlaka hadi Kusini mwa Ulimwengu, kuondoa ukoloni kwenye michakato yake ya Uajiri na Udhibiti wa Wafanyakazi na kukuza uongozi wa Kusini. OiA imejitolea kuwa na mazungumzo ya uaminifu na wafanyakazi kuhusu ahadi za shirika lao, na kushiriki maoni na Shirika kuu la Oxfam. Kwa kuzingatia azma kubwa iliyoainishwa katika mkakati huu, OiA itazingatia kufanya ukaguzi wa ujuzi ili kuhakikisha kuwa ujuzi unaohitajika unapatana na azma hii, hasa masuala yanayoingiliana ili kuiwezesha utekelezaji wa jukumu lake la uongozi.

## Kuchangisha fedha za ufadhili

OiA itawekeza katika uwezo na mbinu za kuchangisha fedha ili kuhakikisha ufadhili wa kutosha na wa miaka mingi wa programu zake. Aina mbalimbali na asili ya majukumu na masuala mbalimbali ya kushughulikiwa katika mkakati huu yanahitaji vyanzo mbalimbali vya ufadhili. Ramani ya wafadhili wa Afrika wote itapewa kipaumbele mwanzoni mwa utekelezaji. Kuongezeka kwa idadi ya watoaji misaada barani Afrika ni fursa kwa OiA kuchunguza, na baadhi ya juhudi kama hizo zinaweza kuongozwa na mashirika ya ndani, ikiwa ni pamoja na Washirika wa Afrika. Ingawa hii inalingana na maadili ya Oxfam kuhusu uongozi wa ndani, uondoaji wa ukoloni na kanuni za kifeministi, kubadilisha mifumo na taratibu za ufadhili kutahitaji juhudi za pamoja. Mpango wa sasa wa Jukwaa la Ushirikiano wa Oxfam ni fursa nzuri ambayo OiA itatumia kusukuma mabadiliko.

## Mkakati wa kampeni

OiA imetoa ahadi ya kufanya kazi kwa njia tofauti, hali itakayohakikisha kwamba mbinu yetu imeondoa ukoloni na kwamba kama timu ya Afrika inayoundwa na vyombo mbalimbali, tunatumia vyema uwezo wetu, nafasi zetu mbalimbali za manufaa na miunganisho yetu ya kimataifa. Tutakuwa wa makusudi katika kuhakikisha kwamba vitendo vyetu vinaendana na ahadi hizi. Kwa hivyo, tumejitolea kutengeneza mkakati wa kina wa kampeni ambao unabainisha ahadi zetu katika ngazi ya kimataifa, matarajio yetu katika mkakati wa OiA, uwezo wetu kama timu, ushirikiano wetu, na rasilimali tunazohitaji ili kuleta mabadiliko tunayotaka kuona. Tutahakikisha tuna ramani ya wazi ya uongozi wa kampeni kama inavyohusiana na shughuli na shabaha mbalimbali za mkakati. Hii itahakikisha utendakazi mzuri na ufaao wa timu ya Afrika na uwasilishaji wa sauti moja katika bara zima.



Djelika ni mkulima huko Bana, Mali. Kabla ya kuanza kwa mradi huo, ardhi aliyotumia kwa muda mrefu ilikuwa imechakaa na wazi kabisa na bila mimea yoyote. Mradi wa Regreening Africa unalenga kurejesha hali ya ardhi baada ya uharibifu wa ardhi kwa kuhimiza wakulima wadogo kupanda miti kwenye mashamba yao na kufufua miti iliyopo. *Picha kwa hisani ya: Diafara Traoré/Oxfam*

# 9.0

# USIMAMIZI WA HATARI

Hatari kuu zinazohusiana na kuwasilisha mkakati wa OiA ni pamoja na vikwazo vya ufadhili, malengo makubwa katika nguzo nyingi yanahitaji usaidizi na ufadhili thabiti wa kifedha. Utegemezi mkubwa wa ufadhili kutoka nje huleta changamoto, haswa ikiwa vipaumbele vya wafadhili vinabadilika au ufikiaji wa njia anuwai za ufadhili unabaki kuwa mdogo. Wafadhali kubadilisha vipaumbele vyao na masuala yao ya kufadhili, hasa katika kukabiliana na mabadiliko ya hali ya kisiasa na kiuchumi na kuongezeka kwa serikali za mrengo wa kulia katika nchi jadi za ufadhili, kunaweza kunyima masuala kama vile haki za kijinsia au haki ya mabadiliko ya hali ya hewa kuzingatiwa kama vipaumbele. Zaidi ya hayo, kukosekana kwa utulivu wa kisiasa na migogoro, hasa katika maeneo kama Sahel, Afrika ya Kati na Pembe ya Afrika, kunaleta hatari kubwa kwa utekelezaji wa programu. Utawala dhaifu, ufisadi na kupungua kwa nafasi ya kiraia katika nchi kadhaa za Afrika kunaweza kudhoofisha zaidi juhudi za utetezi. Hatimaye, OiA inakabiliwa na hatari ya ndani ya kushindwa kuvutia na kuhifadhi wafanyakazi wenye uwezo ili kuendeleza mikakati yake.

Ili kupunguza hatari hizi, OiA itafuata mbinu iliyoainishwa katika hati ya Mchakato wa Mapitio ya CSA 2024 (na hati zilizofuata), ambayo inaangazia mbinu iliyopangwa ya utambuzi wa hatari, tathmini na usimamizi. Mbinu hii hutumia mfumo wa Kudhibiti kwa Kujitathmini (CSA), ambayo inahimiza tathmini endelevu ya udhihirisho wa hatari na ufanisi wenye udhibiti. Mbinu ya CSA inahusisha kugawa majukumu ya utambuzi wa hatari na kugawa sehemu ya upunguzaji wa hatari kwa idara na nguzo za kiufundi kama vile idara za Uendeshaji shughuli, Rasilimali Watu, Mawasiliano na Ufanisi wa Programu. Zaidi ya hayo, mkakati unasisitiza ujumuishaji wa CSA kwa kutumia zana zilizopo, kama vile mikutano ya usimamizi ya ukaguzi wa ubora (QMR) ya nchi, makundi na vitengo na maeneo, ili kurahisisha michakato, kuhakikisha uhifadhi sahihi wa hati na kuimarisha muunganisho kati ya mifumo ya udhibiti wa hatari.



Caroline Nyirenda, Mhudumu wa Afya kutoka Zahanati ya Chawama, akionekana akielimisha jamii jinsi ya kutumia mifuko ya Kuweka Maji ili Kurudisha Maji mwilini kwa jamii za watu waliotengwa wakati wa mlipuko wa kipindupindu huko Lusaka, Zambia tarehe 12 Januari, 2024. *Picha ni kwa hisani ya : Loliwe Phiri / Oxfam*

# HITIMISHO

Ukiongozwa na *Ubuntu*, Mkakati wa Oxfam Barani Afrika 2025–2030 unalenga kushughulikia visababishi vikuu vya ukosefu wa usawa kwa nia ya kuchangia katika kuibuka na Afrika yenye haki.

Mkakati wetu umeundwa kwa ajili ya kuchukua hatua na unalenga kuondoa ukosefu wa usawa katika mamlaka na utawala unaochochea ukosefu wa haki. Tunakubali kwamba katika kipindi cha miaka sita ijayo, mahitaji ya Afrika yatabadilika. Ili kuhakikisha kuwa mkakati unasalia kuwa muhimu na wenye athari, mkakati wetu utabadilika huku tukidumisha upatanishi na matokeo tunayotaka. Tutashirikiana kwa karibu na jamii wenyeji, kuboresha mkakati wetu na kuufanya kuwa thabiti na wenye ufanisi.

Ahadi yetu mpya ni kuchangia kikamilifu kwa Afrika iliyo na usawa. Tunalenga kuendeleza juhudi katika haki za kijinsia, hatua za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, hatua za usaidizi wa kibinadamu, utawala unaowajibika na jumuishi pamoja na haki za kiuchumi. Tutaupa kipaumbele uwazi, haki na ujumuishaji wa jamii, na kupaza sauti zisizowakilishwa au zenye uwakilishi mdogo.

Tunatazamia kuona kile kilicho mbele, na tumetiwa moyo na uwezo wa Afrika na nguvu za watu wake. Licha ya changamoto, tuna matumaini kuhusu kuleta mabadiliko ya kudumu na ya kujitolea kwa ajili ya kuibuka na bara lenye ustawi na linaloongozwa na haki.

Tukiletwa pamoja na kuungana wote kwa ajili ya OiA, tukiiungwa mkono na Shirika pana la Oxfam, tunakabiliana na changamoto hizi sio tu kama mfululizo wa malengo yakuafikiwa lakini kama mabadiliko ya kuelekea Afrika yenye usawa zaidi. Mkakati wetu unasimama kama dhamira ya kubadilisha masimulizi ya Afrika, tukiwa na imani kwamba tuna zana, watu na washirika sahihi wa kugeuza ukosefu wa usawa kuwa jambo la zamani barani Afrika.



Asha Vicky ni mkimbizi wa Sudan Kusini anayeishi katika makazi ya Imvepi Kaskazini mwa Uganda. Vicky, mama wa watoto wawili mlezi pekee asiye na mwenzi, labda ndiye mama mwenye nguvu zaidi ulimwenguni. Vicky anaweza kufanya kazi shambani kuanzia saa 12 asubuhi, kabla ya kwenda sokoni kuuza viungo vya vyakula. Anapata nguvu za kucheza na watoto wake na pia ana motisha ya kuendelea kupanua biashara yake ndogo. *Picha ni kwa hisani ya : Credit: Hans Bach / Oxfam*

# VIDOKEZO

[1] Oxfam (2022). Ahadi ya Kupunguza Kielezo cha Kukosekana kwa Usawa: Africa Briefing.
[2] Franz Fanon (1961). Les Damnés de la Terre. Matoleo ya Maspero
[3] Takwimu. https://www.statista.com/statistics/265759/dunia - idadi ya watu - kwa - umri - na - eneo/
[4] Oxfam (2022). Ahadi ya Kupunguza Kielezo cha Kukosekana kwa Usawa: Africa Briefing.
[5] Umoja wa Afrika. Agenda 2063, toleo maarufu, toleo la Mei 2016.
[6] Oxfam barani Afrika itakuza uhusiano mkubwa na Kundi la Afrika Kaskazini, ingawa ni sehemu rasmi ya eneo la Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini (MENA).
[7] Wakati wa kuandaa mkakati huu, michakato ya ushirika inaendelea kwa Kenya na Senegal.
[8] Ufadhili unamaanisha kuwa maamuzi yanapaswa kufanywa kwa ukaribu iwezekanavyo kwa kiwango cha utekelezaji, huku mstari wa usimamizi ukiingia tu wakati masuala hayawezi kutatuliwa katika ngazi ya ndani zaidi.
[9] Idara ya Utafiti wa Takwimu (2024, Machi 22). Utabiri wa jumla ya idadi ya watu barani Afrika 2020-2050.
[10] UNDP (2020). AHADI YA AFRIKA: UNDP Yarekebisha Ofa ya Kimkakati Barani Afrika.
[11] Idara ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Kiuchumi na Kijamii, Idara ya Idadi ya Watu (2019). Matarajio ya Idadi ya Watu Duniani 2019.
[12] J. Baier na H. Kristofer (2018). Afrika: Mstari wa Mwisho wa Kutokomeza Umaskini Uliokithiri. Maendeleo ya Baadaye.
[13] UNECA. Ripoti ya Uchumi kuhusu Afrika 2021.
[14] ILO (2018). Wanawake na Wanaume katika Uchumi Usio Rasmi: Picha ya Kitakwimu. Toleo la Tatu.
[15] UNCTAD. Ripoti ya Maendeleo ya Kiuchumi barani Afrika 2022.
[16] Kundi la Benki ya Maendeleo ya Afrika (2021). Kuinua Shughuli ya Kilimo barani Afrika.
[17] Ibid.
[18] Cornelli na wengine. (2023). Jinsi ya kuepuka Mgogoro wa Madeni katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. IMF.
[19] Civicus Monitor (2022). Nguvu ya Watu chini ya Mashambulizi. https://civicusmonitor.contentfiles.net/media/documents/GlobalFindings2022.pdf
[20] Afrobarometer (2023, Jan 19). Waafrika wanataka demokrasia zaidi, lakini viongozi wao bado hawasikii. https://www.afrobarometer.org/publication/pp85-Waafrika - wanataka - zaidi - demokrasia - lakini - viongozi wao bado - hawasikii /
[21] Umoja wa Afrika na Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (2019). Ripoti ya Uhamiaji Afrika: Kupinga Simulizi.
[22] Machnet (2023). Mitindo ya Utumaji Pesa Barani Afrika.
[23] GSMA (2023). Uchumi wa Simu za Mkononi Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara 2023 . https://www.gsma.com/mobileeconomy/wp-content/uploads/2023/10/20231017-GSMA-Mobile-Economy-Sub-Saharan-Africa-report.pdf (imepitiwa tarehe 13 Machi 2024)
[24] Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Mwakilishi Mkuu kwa Nchi Zilizoendelea Chini, Zisizo na Bandari zinazostawi Nchi na Nchi za Visiwa Vidogo zinazoendelea. Uwezo wa Vijana, Ufunguo wa Maendeleo Endelevu ya Afrika.https://www.un.org/ohrlls/news/young-people%E2%80%99s-potential-key-africa%E2%80%99s-sustainable-development (accessed 13 March 2024)
[25] Kitengo cha Ujasusi cha Mchumi. Kupima kuenea kwa unyanyasaji wa mtandaoni dhidi ya wanawake. https://onlineviolencewomen.eiu.com/ (imepitiwa tarehe 13 Machi 2024)
[26] Viashiria vya Maendeleo ya Dunia. https://www.un.org/ohrlls/news/young - people%E2%80%99s - uwezo - muhimu africa%E2%80%99s - endelevu - maendeleo (imepitiwa tarehe 18 Machi 2024)
[27] Ibid.
[28] Mtandao wa Taarifa za Usalama wa Chakula na Mtandao wa Kimataifa Dhidi ya Migogoro ya Chakula (2020). Ripoti ya Kimataifa ya 2020 kuhusu Migogoro ya Chakula.
[29] JM Powell na CL Thyne (2011). Matukio ya kimataifa ya mapinduzi kutoka 1950 hadi 2010: Seti mpya ya data. https://www.uky.edu/~clthyn2/powell - thyne - JPR - 2011.pdf (imepitiwa tarehe 19 Machi 2024)
[30] Saa za Matumizi ya Serikali. https://www.governmentspendingwatch.net/ (data iliyofikiwa mnamo 2022)

[31] Hifadhidata ya Matumizi ya Kijeshi ya SIPRI (data ilifikiwa mnamo 2022)
[32] FAO/AUC/ECA/WFP (2023). Muhtasari wa Kanda ya Afrika wa Usalama wa Chakula na Lishe – Takwimu na Mienendo 2023.
[33] GPE (2019). Haki za Wasichana za Elimu: Viongozi wa Kimila na Dini wa Kiafrika Wajitolea Kubadilisha Mawazo.
[34] F. M'Cormack-Hale, J. Patel and N. Ndiaye Diouf (2023, Nov 21). Kupambana na unyanyasaji wa kijinsia kunaongoza ajenda ya Afrika ya haki za wanawake. Usambazaji wa Afrobarometer No. 736. https://www.afrobarometer.org/wp - content/uploads/2023/11/AD736 - PAP4 - Kupambana - kulingana na jinsia - unyanyasaji - vichwa - Afrika - ajenda - kwa - wanawake - haki - Afrobarometer - 18nov23.pdf (imepitiwa tarehe 27 Machi 2024)
[35] Neno 'Ulimwengu wa Walio Wengi', lililoletwa na Shahidul Alam, mwandishi wa picha wa Bangladeshi, mwanaharakati na mwandishi, linatoa angalizo kwenye kukosekana kwa usawa kati ya mataifa yenye watu wengi, mataifa yenye maendeleo duni kiuchumi na 'nchi chache zilizoendelea' zenye nguvu. Ingawa mara nyingi hutumiwa kwa kubadilishana na 'Global South', thamani yake iko katika kutoa changamoto kwa masimulizi ya katikati ya Ulimwengu wa Kaskazini, na utambuzi na uthamini wa mali ya kipekee ya Ulimwengu wa Walio Wengi, hasa katika nafasi za kimataifa.
[36] OiA itatoa kipaumbele kwa ushirikiano na RECs nane zinazotambuliwa na AU: Muungano wa Arab Maghreb (UMA) (kupitia Cluster ya Afrika Kaskazini), Soko la Pamoja la Mashariki na Kusini mwa Afrika (COMESA), Jumuiya ya Nchi za Sahel–Sahara (CEN–SAD), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika ya Kati (ECCAS), Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi. (ECOWAS), Mamlaka ya Kiserikali ya Maendeleo (IGAD) na Kusini mwa Afrika Jumuiya ya Maendeleo (SADC). Uhusiano na RECs nyingine pia utaendelezwa kulingana na hitaji la kimkakati.
[37] Umoja wa Afrika (2023). Muhtasari wa Azimio la Viongozi wa Afrika la Nairobi kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi na Wito wa Kuchukua Hatua. Mkutano wa Kilele wa Hali ya Hewa barani Afrika tarehe 4 -6 Septemba 2023 Nairobi, Kenya. https://au.int/sites/default/files/documents/43682 - hati - AU_Nairobi_Declaration_Action_1.pdf
[38] IASC. The Grand Bargain (Tovuti rasmi). https://interagencystandingcommittee.org/grand bargain
[39] Charter4Change. Ujanibishaji wa Misaada ya Kibinadamu. https://charter4change.org/
[40] Ahadi ya Mabadiliko. https://pledgeforchange2030.org/



OXFAM